Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 31 Machi, 2015

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani kuhusu uwasilishaji wa Kauli ya Serikali juu ya upungufu wa mafuta ya petroli Zanzibar. Naomba kuwasilisha.

KAULI YA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, hivi karibuni kumejitokeza upungufu wa mafuta ya aina ya petroli hapa nchini, jambo ambalo linasababisha kudhorota kwa huduma za usafiri wa vyombo vya baharini na kuwasababishia usumbufu wananchi wetu. Kutokana na hali hii, serikali imeona ni vyema kutoa taarifa kwa wananchi kuwaelezea hali halisi ilivyo na jitihada zinazochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na wafanyabiashara wa bidhaa hii ili kuondoa tatizo hili.

Mhe. Spika, serikali imefuatilia tatizo hilo na kugundua kwamba zipo sababu tatu kuu zilizopelekea kutokea upungufu wa bidhaa ya petroli hapa nchini. Sababu hizo ni kama zifuatazo:

Moja, gati inayotumika kupitishia mafuta huwa na kina kidogo cha maji, hivyo hupelekea mafuta yanayoletwa nchini kuletwa na meli ndogo na kwa kiwango kidogo. Mahitaji ya mafuta hivi sasa yameongezeka sana kutokana na watu wengi kutumia na kumiliki vyombo vya usafiri, hivyo mahitaji hayo yanazidi kiwango cha mafuta yanayoingizwa nchini.

Pili, kwa kawaida kampuni za mafuta hapa nchini huchukua mafuta kutoka Dar es Salaam na Mombasa nchini Kenya. Kampuni ya *GAPCO* inachukua mafuta yake kutoka Dar es Salaam, Kampuni ya *Zanzibar Petroleum* na *United Petroleum* zinachukua mafuta yao Mombasa. Kwa bahati mbaya kumejitokeza tatizo la mahitaji haya sana, hivyo foleni zimesababishwa na meli kuingia gatini katika bandari zote mbili. Tatizo hili hupelekea meli za kuchukulia mafuta ya Zanzibar nazo kukaa foleni zikisubiri zamu. Mara kadhaa kampuni za mafuta zimekuwa zikiiomba serikali kuwasiliana na Serikali ya Kenya kuomba meli ya Zanzibar ipewe kipaumbele. Serikali imekuwa ikifanya hivyo mara kwa mara ili kupatikana mafuta hayo mapema iwezekanavyo.

Naomba kuchukua fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Kenya kupitia wizara yake ya Nishati, Mamlaka ya Bandari ya Kenya na Mamlaka ya Mapato ya Kenya kwa kusikiliza maombi yetu na kusaidia kila inapowezekana linapojitokeza tatizo hili.

Tatu, hivi sasa pia kumetokea mabadiliko ya utaratibu wa ununuzi wa mafuta. Utaratibu mpya uliopo Tanzania Bara na Kenya ni kwamba Kampuni ya Mafuta kuingiza mafuta kwa kutumia muingizaji mmoja (*block procurement system)* na kutoa mahitaji yao kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu. Utaratibu huu nao umejitokeza kuwa na changamoto kwa kampuni za Zanzibar kwani inawawia vigumu kuuziwa mafuta yaliyoingizwa kwa ajili ya kipindi maalum kwa soko lililokusudiwa.

Mhe. Spika, matatizo haya yanahitaji kushughulikiwa ili kuondoa tatizo la upungufu wa mafuta unaojitokeza kutokujirejea rejea. Serikali itashirikiana na makampuni yanayoingiza mafuta nchini kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili. Hata hivyo, matatizo mengine kama vile ya kuongezeka kina cha maji katika eneo la kupokelea mafuta hapo Mtoni yanataka muda wa kati au mrefu kuyatatua, ili kuruhusu meli kubwa zaidi ziweze kuingia eneo hilo na kuleta mafuta kwa wingi zaidi.

Mhe. Spika, pamoja na changamoto nilizozitaja, serikali imekuwa ikifuatilia na kusimamia upatikanaji wa bidhaa hii muhimu, na tatizo sasa tumehakikishiwa kuwa tayari jumla ya lita milioni mbili laki sita tisini na nane elfu na mia mbili (2,698,200) za mafuta ya petroli yamepakiwa na yanatarajiwa kuingia nchini na kujazwa kwenye visima leo hii tarehe 31/03/2015. Hivyo, ifikapo kesho tarehe 01/04/2015 matarajio ni kwamba kutakuwa hakuna tatizo la mafuta nchini, na serikali itafuatilia kwa karibu ili kwa kadiri inavyowezekana kuepusha tatizo hili lisijitokeze tena.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunawashukuru sana wananchi wote kwa kuwa wastahamilivu katika kipindi chote cha upungufu wa bidhaa hii muhimu na tunawapa pole kwa usumbufu uliotokea.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tunakushukuru na kama tunavyoelewa kwamba masuala yanayoangukia chini ya kauli ya mawaziri au kauli ya serikali huwa hayajadiliwi, ila hupewa nafasi Mwenyekiti wa Kamati aweze kusema maneno kwa niaba ya kamati na hatimaye Spika kama maswali yapo anaweza kuchukua mawili matatu na baadae kumwita waziri ili kufunga taarifa hii.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, sina budi kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kutuwezesha siku hii ya leo tukaamka salama na hatimaye tukaweza kufika hapa kuendelea katika mambo ambayo huwa tunayapanga kila siku.

Mhe. Spika, mimi kwa siku ya leo sina mengi sana ya kuzungumza hususan ukitilia maanani kwamba hili suala ambalo lilikuwa linatusumbua kwa muda mrefu na tulipokuwa tunataka kauli ya serikali hatimaye serikali leo imeweza kuja kutoa kauli hii. Tunakubali na utaratibu ambao tayari umekwisha kubadilika katika maeneo ambayo mafuta yanapatikana kwa sasa, tulijaribu kufuatilia na tumepata maelezo kama ambavyo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais amekuja kuwasilisha hapa. Sasa kwa upande wetu sisi kamati tunasema kwamba tunashukuru sana.

Vile vile tunaiomba serikali ihakikishe kwamba inatengeneza utaratibu makini ili suala hili lisije likatokezea tena kama vile ambavyo Mhe. Waziri amekwishakutwambia. Tunashukuru sana kwa hilo na tunasema kwamba tujitahidini na tunaomba wananchi wawe wastahamilivu na suala hili *Inshaallah* kesho litakuwa limemalizika.

Ahsante Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, kuna nafasi chache za maswali kwanza tumsikilize Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nichukue nafasi hii nikushukuru kwa dhati kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza swali langu dogo kutokana na taarifa hii ya serikali. Kabla sijauliza swali hili nikuombe pia nitoe neno dogo sana la sekunde mbili tatu nalo ni la shukurani tu, kuishukuru serikali kwa taarifa hii waliyoitoa ambayo itapata kuwasaidia wananchi wetu kujua tatizo halisi lililojitokeza na niseme kwa bahati nzuri nawapongeza serikali. Kwa sababu mimi mwenyewe jana niliamua kutaka kuleta hoja yangu ya dharura kutaka kujua kadhia hii, lakini hoja yangu ile haikupata nafasi. Naishukuru serikali na nimeridhika baada ya serikali kutoa taarifa yake hii.

Mhe. Spika, swali langu nataka niulize, kwa kuwa suala la kuingiza mafuta kwa kutumia uingizaji wa mtu mmoja, yaani *block procurement system,* nilitaka kujua utaratibu huu umeanza muda gani hata usumbufu uanze leo. Hiyo (a).

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa katika majibu ya serikali au taarifa ya serikali imeeleza kwamba kuna tatizo la kina kidogo cha maji katika eneo la kushushia mafuta, nilitaka kujua kwa kuwa tatizo hili linaweza likachukua muda mrefu. Je, serikali ina mipango gani ya matayarisho ili kuweza kukabiliana na suala hili lisije likajitokeza tena mara kwa mara, baada ya mafuta ambayo yanategemewa kuingia leo. Mheshimiwa nakushukuru.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa nikauliza swali dogo. Kwa kuwa hili tatizo la mafuta halijajitokeza hizi siku mbili, tangu mafuta yaliposhushwa bei siku ya kwanza, siku ya pili ukienda kwenye vituo vya mafuta unaambiwa hapana, siku ya tatu yapo, ukikaa tena siku mbili mafuta hapana, siku ya tatu unayakuta, inakuwa hili ni tatizo tangu siku yaliyopunguzwa bei mafuta haya kuna tatizo la kujitokeza mara kwa mara vituoni kwa kuadimika mafuta haya.

Je, Mhe. Waziri kwa suala hili atatwambia nini.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa hii nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja. Moja ya sababu alizosema zinazopelekea upungufu wa mafuta...

Mhe. Spika: Kama kuna simu hebu tuizime hapo ili tuweze kusikilizana vizuri. Mheshimiwa endelea.

Mhe. Marina Joel Thomas: Alisema moja ya sababu ni mahitaji ya mafuta yameongezeka sana kutokana na watu wengi kumiliki vyombo vya usafiri, hivyo mahitaji hayo yanazidi kiwango cha

mafuta yanayoingizwa nchini. Labda nimuulize Mhe. Waziri umiliki wa vyombo sasa hivi wa magari umekuwa mwingi mno hapa nchini, na ukiangalia nchi yetu ni ndogo na kila siku uingizwaji wa magari umekuwa mwingi bila ya mpangilio.

Je, serikali ina mikakati gani kudhibiti uingizwaji wa magari, kwa sababu itakuwa kama Dar es Salaam mtu anaweza akaenda Malindi akachukua zaidi ya masaa matatu au manne. Je, serikali inaonaje suala hili.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali langu dogo. Kutokana na ukosefu wa mafuta imeonekana na vijana wengi kuuza mafuta kwenye mageloni. Je, serikali ina mpango gani wa kupiga vita suala hili.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi, vile vile niishukuru serikali kwa kuweza kutoa taarifa hii. Lakini katika taarifa hii imeelezwa kwamba zile kampuni ambazo zinaleta mafuta ni kampuni tatu ikiwemo *GAPCO, Zanzibar Petroleum* pamoja na *United Petroleum.* Sasa swali langu ni kwamba, pengine kampuni hizi tatu zinazoleta hakuna kampuni nyengine ambayo ishawahi kuomba kuleta au kuagiza mafuta ili kuondoa tatizo hili, pengine upungufu wa kampuni hizi chache kuweza kuleta tatizo hili. Je, serikali kuna mambo yoyote ya kampuni nyengine ambayo imejitokeza, na kama haipo kuna utaratibu gani kuangalia kwamba kuweza kutafuta kampuni nyengine na kuweza kuondoa tatizo hili la mafuta.

Mhe. Spika: Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe naomba nimwite tena Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kutoa maelezo juu ya maswali yaliyoulizwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kujibu maswali ambayo Wajumbe wameyaleta mbele ya Baraza lako Tukufu.

Kabla ya kufanya hivyo niwatambue Waheshimiwa Wajumbe sita ambao waliwasilisha maswali yao. Nianzie kwa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Bikame Yussuf, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Shadya Mohammed Suleiman na Mhe. Nassor Salim Ali maarufu Jazira.

Mhe. Spika, nikianza kwa Mhe. Mahmoud Muhammed yeye alitoa ushauri kwamba zichukuliwe jitihada na kuwe na utaratibu ulio makini zaidi ili tatizo hili lisijirudie.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe nia na madhumuni ya serikali ni kuhakikisha kwamba kila tatizo linapata ufumbuzi ili tatizo lisitokee, linapotokea linakuwa ni kwa bahati mbaya na wakati mwengine ni zaidi ya hali ambayo inakuwepo wakati huo. Kwa hivyo, nia na madhumuni na dhamira ya serikali ni kuchukua kila jitihada ili tatizo hili lisiweze kujirudia kama ambavyo limejitokeza.

Kwa hivyo, katika kipindi ambacho tutakuwa tunachukua hatua hizo; kwa sababu ziko za muda mfupi na muda mrefu, ningeomba tuendelee kustahamiliana pale ambapo litatokea, lakini

dhamira yetu ni kuondosha tatizo hili. Tutajitahidi kusikiliza ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe ili tatizo hili lisijirudie rudie.

Mhe. Ali Salum Haji ametaka kujua utaratibu huu wa *block procurement system* umeanza muda gani. Utaratibu huu upo kitambo kidogo na si kwa Zanzibar tu, utaratibu huu ni kwa upande wa Tanzania Bara na Kenya ambapo sisi ndio tunanunua mafuta yetu huko. Kwa sababu ya soko la Zanzibar ni dogo, wenzetu hawa wameweka utaratibu huo kwa sababu ya mivutano mikubwa iliyokuwa ikijitokeza hasa hasa katika kukwepa kodi kwa waletaji mafuta. Ndio maana ukaweko huu utaratibu wa uagizaji wa kutoa *tender* mtu mmoja mmoja ili serikali husika ziweze kufuatilia ziweze kupata mapato yake na ziweze kuona mafuta yanayoingia nchini yametimiza viwango. Kwa sababu kulikuwa na udanganyifu mkubwa wa kuchanganya maji na mafuta na mengine na yalitokezea hapo nyuma na magari yetu mengi yalipata matatizo.

Sasa katika kutatua tatizo hili ndio ikaja hii *block procurement system* kwa wenzetu wa Tanzania Bara na wenzetu wa Kenya. Sasa sisi kwa Zanzibar hatuna utaratibu huu, mwenye uwezo wa kuleta mafuta hakatazwi ilimradi ametimiza yale masharti. Na masharti makubwa ya hapa Zanzibar ya kuleta mafuta uwe na *storage facilities* tujenge yale matenki ya kuwekea mafuta, maana mafuta sio kama bidhaa ya kawaida utasema mjomba niwekee, yakiripuka hapakaliki hapa, kisiwa chote hakipo.

Kwa hivyo, lazima kuwe na utaratibu maalum ambao unasaidia katika kuhakikisha hali ya nchi inakuwa salama na uletaji unafuata masharti ili wananchi waweze kupata mafuta bila ya kuathiri nchi yetu.

Kuhusu kina kidogo cha maji Mheshimiwa sote tunapajua Mtoni kila baada ya muda fulani pale kwenye Bandari yetu inayosimama meli hujaa mchanga pale. Kwa hiyo, uwezo wa meli kubwa kufunga gati pale unakuwa mdogo. Kwa hivyo, serikali ina utaratibu wa kutaka kufanya ili Bandari ile iweze kufikika vizuri na meli zilizo kubwa zaidi, lakini pia wako wafanyabiashara waliojitokeza ambao wanataka wao sasa wajenge hizi bandari maalum za kuwekea haya mameli makubwa.

Kwa hiyo, mazungumzo na serikali yanaendelea na pale mambo yatakapokuwa vizuri basi tutangalia ni utaratibu upi uliokuwa mzuri ili ufanyike kuondosha tatizo hili. Kwa sasa kwa dharura tutaendelea kushughulikia na bandari yetu iliyoko pale Mtoni ili kupata hatua za dharura zitakazowezesha meli zilizokuwa kubwa kidogo ziweze kufunga gati tatizo hili liweze kuondoka.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad anasema tatizo limejitokeza mara tu baada ya bei ya mafuta kushuka. Sasa inawezekana, kwa sababu sasa bei iliposhuka ya mafuta inawezekana wanunuzi wamekuwa wengi wa mafuta na ndio maana Bandari ya Mombasa imejaa mameli ya mafuta, Bandari ya Dare es Salam imejaa, kila mmoja anataka anunue mafuta wanakimbilia kununua kwa sababu wanahisi pengine mafuta yanaweza kupanda bei. Sasa kila mmoja ananunua.

Sasa sisi kwa sababu hatuwezi kununua kwa *content* kubwa, kwa sababu huna Bandari ya kutosha ya ku- *share* mafuta, tunanunua kwa *content* ndogo yanakwisha upesi na mahitaji

yanakuwa makubwa nchini mwetu, tushukuru Mungu ndio maendeleo hayo. Kwa hivyo, yanapojitokeza matatizo yanasababishwa pia na hali halisi ya maendeleo ya nchi yanavyojitokeza; magari yamekuwa mengi, mahitaji yamekuwa mengi, ujenzi umekuwa mkubwa na shughuli zimekuwa nyingi, watalii wamekuwa wengi, zote ni neema. Kwa hiyo, tuombe Mungu neema hii izidi mahitaji ya mafuta yaongezeke, tujipange vizuri nchi iwe na harakati za kiuchumi tupige hatua kubwa zaidi.

Mhe. Marina Joel Thomas alitaka kujua ni mpango gani tutauchukua ili kudhibiti uingiaji wa magari nchini. Hivi sasa serikali imeweka mpango maalum wa kudhibiti yale magari machakavu kwa kuongeza kodi ili kupungua uingiaji wa magari nchini, kwa msingi kwamba tusilete magari yaliyokwishachakaa kwa utaratibu huo kwa njia moja au nyengine unasaidia.

Lakini vile vile magari yanayoingia nchini sio tu yanatumika hapa, wafanyabishara wetu pia inawasaidia na inapowasaidia wafanyabiashara pia zinasaidia na kodi za nchi na harakati za kiuchumi zinakuwa. Kwa hivyo, yale magari mengine yanayokuja ambayo yametimiza vigezo tuyaachie yaingie yatakayotumika ndani yatumike na yale ambayo yatasafirishwa kupelekwa nchi nyengine yakauzwe basi yakauzwe ili faida ya nchi ipatikane.

Cha msingi hapa ni hizi hatua zinachukuliwa na serikali za kuongeza kujenga miundombinu ikiwemo ya barabara, kadiri tunavyojenga barabara nyingi na kupanua barabara zetu inasaidia kuondosha msongamano. Cha msingi tusiogope kuingia kwa magari, tujitayarishe kwa kuingia kwa magari kwenyewe, kwa sababu ndio maendeleo, watu leo kila mmoja anataka gari yake atembee kwa gari yake, lakini jitihada kuwa ni kujipanga kujenga miundombinu iyakayosaidia kurahisisha usafiri ili kupunguza kuingia kwa magari nchini tuanze na sisi kuwa na *trains* zetu na *public buses* zile na usafiri wa umma huu wa magari ya kisasa na matreni yanayokwenda kisasa, na mji wetu tuujenge vizuri tuendelee tuwe na sisi Zanzibar iwe Dubai ya pili hapa na tusiwe kama tulivyo. Kwa hivyo, tujitahidini kila ikitokea neema ya kuhamasisha maendeleo ya nchi tusiyaogope, tujitayarishe kuogelea nayo ili twende mbele zaidi na nchi yetu iweze kupiga hatua zaidi.

Mhe. Spika, suala la 5 la Mhe. Shadya Mohammed Suleiman sikulisikia kwa sababu humu dani mwetu ukiwa husemi na spika hii matokeo yake husikilikani. Kwa hiyo, nitamuomba alirudie isipokuwa nimalizie la Mhe. Nassor Salim. Je, kuna kampuni ambazo zinataka kuleta mafuta lakini pengine hazikupewa ruhusa au hazijajitokeza.

Zipo kampuni zilizojitokeza, zipo lakini unapojitokeza lazima ufuate yale masharti yaliopo na sharti letu kubwa ni kuwa na *storage facilities,* kuwa na pahala pa kuwekea mafuta na kama huna mahali pa kuwekea mafuta hayo hicho ni kikwazo, hatukupi, maana hatari yake ni kubwa sana.

Hatari yake kama hakuna udhibiti wa kuyaweka vizuri mafuta katika sehemu zilizoruhusika, matokeo yake kisiwa hakipo, maana mfano ikitokea kwa kuungua kwa moto na lolote au jambo lolote athari yake ni kubwa sana. Haiwi mnaona kwa mfano pale yanapoadimika mafuta

tunapoweka vigeleni viwili vitatu ndani ya majumba yetu ikitokea athari yake huwa kubwa sana, Je, mamilioni ya *litres,* Mungu atuepushie mbali uje uyaweke ovyo ovyo yaripuke itakuwa ni balaa kubwa.

Kwa hivyo, hazikatazwi kampuni kuleta mafuta alimradi zimefuata sheria na taratibu za nchi na zimetimiza vigezo. Kwa hiyo, tunawakaribisha wawekezaji hususan katika eneo hilo waende kwa wahusika Wizara ya Fedha wazungumze nao, ili kama wanahitaji kuleta wakamilishe masharti yanayotakiwa na waweze kuleta mafuta nchini. Mhe. Spika, sasa naomba Mhe. Shadya Mohammed arudie swali lake ili tuweze kumjibu.

Mhe. Spika: Mhe. Shadya Mohammed Suleiman naomba urudie lile swali lako halikusikika vizuri kwa Mhe. Waziri na Wajumbe tunaomba urudie lile swali.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, kutokana na ukosefu wa mafuta kumeonekana vijana wengi kuuza mafuta kwenye mageleni, hii ni hatari hata kuhatarisha vyombo vya wananchi. Je, serikali ina mpango gani wa kupiga vita suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nimelisikia sawa anaulizia kwamba kutokana na upungufu wa mafuta kumejitokeza vijana kuuza mafuta nje ya utaratibu wa kawaida wa mafuta. Je. serikali ina mpango gani kuzuia biashara hii haramu isiendelee, watu wasiuze mafuta vichochoroni.

Ni kweli Mhe. Spika, hairuhusiwi, ni kosa tena ni kosa kubwa sana kuuza mafuta kiholela holela na hatari yake kama nilivyosema yanapotokea majanga ya mafuta mitaani huko balaa lake ni kubwa sana, lakini pakeshakutokea upungufu watu huujaza upungufu huo kwa kutafuta aina mbali mbali za mambo.

Kwa hivyo, tamko langu ninalosema hapa Jeshi letu la Polisi ambalo ndio linapewa dhamana kisheria kushughulikia aina yoyote ya uhalifu iwashughulikie pia hawa ili wawapeleke katika vyombo vya sheria na sheria ichukue mkondo wake.

Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri amekamilisha kutoa kauli ya serikali tuone kiasi gani taarifa hii Wajumbe mumeipokea pamoja na yale maelekezo muliyoyatoa. Wale wanaokubali kupokea taarifa hii pamoja na maelekezo kwa serikali wanyanyue mikono, wanaoikataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Hoja ya kuitaka serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kuwapatia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi

(*Majadiliano yanaendelea*)

Mhe. Spika: Waheshimwia Wajumbe majadiliano yanaendelea, na kwa mujibu wa taarifa niliyopewa na Mhe. Naibu Spika, kuna jumla ya Wajumbe karibu 27 walikwishachangia na Wajumbe wa safu ya nyuma wamebakia Wajumbe 3 akiwemo Mjumbe mmoja aliyebakiza dakika 5. Safu ya mbele kwa maana ya mawaziri, mawaziri jumla yao kuna 10 hii inafanya idadi ya kutosha sana ya jumla ya Wajumbe 40 wamechangia hoja hii.

Kwa hiyo, kwanza niseme kwamba idadi hii inatosha sitaki zaidi na nadhani itakuwa tumepata mwanga wa kutosha katika mjadala huu. Kwa hiyo, sihitaji zaidi ya hawa. Kwa hiyo, kwa kuendelea na majadiliano naomba nimkaribishe Mhe. Salma Mohammed Ali amalizie dakika 5 halafu afuate Mhe. Rufai Said Rufai wakati Mhe. Hamza Hassan Juma anajitayarisha na pia Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa naye anajitayarisha ndio ile safu ya nyuma ile, tuendelee.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumalizia dakika zangu tano zilizobakia.

Mhe. Spika, naomba nianze katika mchango wangu katika vitambulisho ambapo tumeambiwa viko vingi vimerundikana na havijaenda kuchukuliwa.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa Wajumbe waliomaliza Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kuna Mjumbe mmoja alisema kama tulitembelea katika Afisi ile na tukavikuta vitambulisho vingi.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya naomba nieke *hansard* sawa, kwa sababu pengine Mjumbe alikwenda na kamati nyengine lakini kamati yetu sisi ya viongozi wakuu wa kitaifa iliyomaliza muda tulizungumza na viongozi wa vitambulisho katika kuthibitisha ratiba na katika utekelezaji wa ripoti ya wizara, lakini hatujawahi kwenda hata mara moja katika Afisi yao ya Vitambulisho.

Mhe. Spika, lakini mimi binafsi, Mhe. Waziri Mhe. Mwinyihaji Mkurugenzi wa vitambulisho Wawakilishi na Wabunge na Madiwani tulikwenda kuthibitisha kadhia hii.

Mhe. Spika, ni kweli tulivikuta vitambulisho lakini kwa bahati moja mbaya au nzuri vile vitambulisho vilikuwa vimefungwa raba bendi na hatukuruhusiwa kuvifungua. Lakini kuna vitambulisho vya Wadi moja ya Chonga Diwani wa viti maalum alivinyanyua, kwa bahati nzuri kitambulisho kilichokuweko juu kilikuwa cha jirani yake na alinambia mimi nikifika nikiteremka gari basi mguu wa mwanzo nitaingia kwenye nyumba hii kumwambia huyu aende akachukue kitambulisho chake.

Mhe. Spika, lililotokezea Diwani yule alikwenda na alipofika alimtaka yule akachukue kitambulisho chake lakini alimwambia kuwa kitambulisho mimi ninacho, akamwambia lete tukione itakuwa kitambulisho kimesha-*expire*. Mhe. Spika, kitambulisho kilitolewa cha mtu yule ambaye kule kipo na jina lake na picha yake na kitambulisho kilikuwa kina muda wa miaka mitatu mbele ku- *expire*.

Mhe. Spika, kwa hili inaonesha kwamba kuna vitambulisho vyengine vimetolewa mara mbili na kuna vitambulisho vyengine waliandikwa watu kwa ile ile tunayosema mambo ya kisiasa wapewe vitambulisho ili wapewe vitambulisho vya kura wapige kura, na bahati mbaya watu walikuwa wa kupandikizwa sasa hawana. Kwa hiyo, vitambulisho vimekaa.

Lakini ikiwa vitambulisho viko kwa nini watu wanakwenda na hawapewi na wana risiti mkononi? Wako watu na ushahidi umetolewa kila siku wanakwenda kutafuta vitambulisho vyao na hawapewi, sasa kwa kweli hili ni tatizo wasikusanye vitambulisho vikatolewa mara mbili mbili watu waliokuwa tukaambiwa kuwa kuna vitambulisho tele watu hawaendi kuchukua, ikiwa vipo wanaokwenda na wapewe au kwa sababu Kombo haendi kuchukua yule Asha anayekwenda kuchukua asipewe. Mhe. Spika, hili haliwezekani.

Jambo jengine ambalo naomba sasa nilizungumzie hapa tumeambiwa kwamba kuna vyeti feki. Mhe. Spika, mimi siwezi kutoa vyeti feki. Hata kama vyeti feki vinatolewa basi vinatolewa huko huko serikalini, mimi Salma sina uwezo wa kutoa vyeti feki. Nakataa kabisa kama kuna vyeti feki, isipokuwa ni mbinu ile ile ya kuwazuia watu kupata haki zao.

Mhe. Spika, hapa katika bajeti ya 2012/13 nilizungumzia kuhusu cheti za mtoto wangu ambaye aliambiwa ni cheti feki. Mhe. Spika, mimi mwanangu wa mwanzo nilimzaa 30/10/1994 na siku niliyomzaa nilipewa kipande hospitali nikakipeleka kwa Mkuu wa Wilaya na baada ya miezi mitatu au minne nilipata cheti, nashangaa mwanangu katimiza miaka 18 naambiwa cheti ni feki.

Cheti kile Mhe. Spika, nilihangaika nacho nikaja Wizara ya Katiba na Sheria sijui mara ngapi nikifika wananambia kuwa cheti ni sahihi lakini nikirudi kule wananambia ni feki.

Mwisho walipojua kuwa ni Mwakilishi walinambia tunakupa tu kwa sababu Mwakilishi lakini cheti chako ni feki. Mimi niliwaambia sitaki kupewa kwa sababu ni Mwakilishi, uwakilishi wangu utamalizika na mwanangu cheti atataka kukitumia siku zote, nataka uhalali wa cheti hichi. Kwa hiyo, Mhe. Spika, hii inaonesha kuwa kuna vyeti vilivyokuwa ni *original* lakini watendaji wanasema kama vyeti ni feki.

Mhe. Spika, naomba nimalizie jana katika mchango wangu niliishia kwa kusema kama Masheha wamepewa mpango maalum wa kuwahangaisha watu ili wakate tamaa kutafuta haki yao na nilitoa mfano lakini katika ule mfano ndipo nilipomalizia.

Mhe. Spika, katika Jimbo la Wawi kuna Sheha mmoja Sheha mikabio. Sheha huyu ana nyumba mbili. Ana kawaida watu wanapomfuatia kutaka fomu za kwenda kutafutia vitambulisho huwaambia njooni siku fulani na nitakuwa nyumba fulani. Sasa ujue siku hiyo hayuko kule huwa anawahangaisha watu na anajua nyumba zake mbili ziko masafa marefu, mtu hawezi kutoka nyumba hii na siku ile ile akaenda nyumba nyengine.

Kwa hiyo, hili ni tatizo lakini mimi siwashangai Masheha. Sheha anafika kumkana mwanawe kwa sababu wana itikadi tofauti za kisiasa. Sheha kwenye uandikishaji anasema mimi mtoto

huyu simjui, mwanawe aliyemzaa au mtoto wa kaka yake Mwenyezi Mungu awasamehe waliotangulia, lakini wapo Masheha wanafanya hivyo. Kwa hivyo, mimi siwashangai isipokuwa ninawashangaa wale wanawake wenzangu waliokuwa wana imani na watoto wao wakaweza kukaa na watu wa aina hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninasema mbele ya Baraza la Wawakilishi siku yoyote mume wangu atakayopewa nafasi ya Usheha, basi ndoa mimi na yeye itamaliza. Kwa sababu ni watu waliokuwa hata umuone na imani gani, siku atakayopewa nafasi ile basi anageuka.

Mhe. Spika, ni jambo fika mtu kumkana mwanawe, mtu anafika kusema mwanawe hamjui kwa sababu wapo tofauti kwenye itikadi zao. Kwa kweli ni tatizo na mtu kama huyo uwe na roho ngumu sana kuishi naye. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo ninakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Makadhi wapo hapa kwamba kauli ya mwanamke haina nguvu katika talaka. *(Kicheko/Makofi).*

Ninashukuru sana. Sasa ni zamu yake Mhe. Rufai Said Rufai na kumekuwa na makubaliano ya kuchangia dakika 10. Kwa hivyo na Mhe. Rufai achukue dakika 10 katika mchango wake afuate baadae Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Rufai Said Rufai: Bismilillahi Rahman Rahim. Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Allah na kumtakia rehma Mtume wetu (*S.A.W*), asubuhi hii kuweza kuwa katika afya pamoja na nyinyi tukaweza asubuhi hii kukutana hapa katika Baraza la Wawakilishi kwa kuzungumzia hoja iliopo mbele yetu ya Mhe. Hamad Masoud Hamad, inayohusu kuitaka Serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki yao ya kupatiwa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi *(Zan-ID).*

Mhe. Spika, hii hoja imejieleza lakini baadhi ya sisi wachangiaji tumo katika kuipotosha hii hoja. Hii hoja inaitaka Serikali kuwatimizia Wazanzibari wale ambao wameshatimiza sifa tena za kisheria. Inavyotaka sheria wapo hao Wazanzibari ambao sifa hizo wanazo. Kwa hivyo, mleta hoja ametaka hawa ambao hizi sifa tayari wanazo, hii haki yao ya kisheria waweze kupatiwa. Kwa yule yeyote ambaye hana hiyo sifa, hii hoja haimuhusu. Kama hao haiwahusu hii hoja hatuna haja sisi kuwatafuta hao. Twende katika wale ambao wamefuata taratibu na sifa wanazo na sheria imewakubali.

Sasa kama kuna watu wanavunja sheria ambayo tumeiandika wenyewe kwa mikono yetu, lakini ikawa sasa tunatafutia namna gani ya kuendeleza kuvunja sheria. Mhe. Spika, itakuwa hivyo hatufanyi wajibu wetu, kwa sababu sheria ya nchi hii haimbagui Mzanzibari wa aina yeyote, lakini inawezekana sasa wasimamizi wa sheria hawafanyi wajibu wao.

Sasa kama kuna watu hawafanyi wajibu wao, tukaja hapa tukasema, ikawa miongoni mwetu sisi Wawakilishi tukasema siyo pahala pa kusema tupeleke kesi Mahakamani, tumefanya nini. Haki ya Wawakilishi mdomo wao ni hili Baraza la Wawakilishi kuwasemea Wazanzibari. Kwa hivyo,

mimi ninahisi kwamba tushikamane kuitetea sheria ya Zanzibar tuliyojiandikia ili iweze kuendeleza majukumu ya nchi hii.

Lakini kwa mwendo tunaokwenda nao Mhe. Spika, aliyekuwa haisimamii sheria tukamfanya anafanya jambo la maana, basi kwa utaratibu huo, tusifikiri kwamba watapata tabu ni hawa tu, hapana na wewe binafsi utakuja kupata jambo ambalo linakulazimu sheria ifanye kazi, wakati mtu umeshamzowezesha hivyo na wewe pia hatakutekelezea.

Mhe. Spika, tumeshuhudia mambo mbali mbali. Kipindi cha uchaguzi 2000 baada ya kutangazwa matokeo katika maeneo mbali mbali, kulitokea kuangushwa miti barabarani, barabara zote zikafungwa, lakini kuna watu walijiona kwamba wao ni wana sisi, wakapita yale maeneo na kwa bahati ndugu zetu wa vyombo vya ulinzi Polisi wakawa yale maeneo tayari wameshafika. Sasa watu kupita wakazuiwa, wakaambiwa haya magogo yote yaondosheni, wakasema aah! sisi ni wana CCM bwana! wakaambiwa nyinyi CCM ndiyo tunaowataka hasa, pakawa na mvutano pale.

Kwa hivyo, ndiyo maana sheria, sheria ikifanya kazi haimuangalii nani. Hivyo ukiwa wewe ni CCM, ukiwa ni CUF ni lazima utapambana nayo. Mhe. Spika, hivyo yakawadhuru haya, na siyo hayo na hata wakati wa ukoloni, ulipoondoka ukoloni ukaja uhuru. Mapinduzi katika kusafisha maeneo kuna wana Afro Shirazi waliambiwa hakuna kutembea, wakasema sisi ni Afro Shirazi gogo, wakapita katika maeneo, kufika kukamatwa na Jeshi, wakasema ooh! bwana! sisi ni wana Afro Shirazi gogo, wakaambiwa huyo Afro Shirazi ndiye tunayemtaka, wakachezea mkong'oto. Kwa hivyo mambo haya tusiyafanye kama ni mambo mepesi, ni lazima haki za watu tuzisimamie.

Mhe. Spika, ...

Mhe. Spika: Una dakika 2.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, tumeona hapa kwamba kuna vijana wengi ambao nikitoa mfano ndani ya jimbo langu lina watu mia moja na sabini na tatu (173), hawa wana miezi sita wameshakuwa na risiti za kupatiwa vitambulisho. Yaani utaratibu wote wa sheria umeshakamilika, miezi sita hawajapata vitambulisho. Tume ya Vitambulisho ilisema ndani ya wiki mbili tu watu waliokwishapiga picha na kupatiwa risiti basi watapewa vitambulisho vyao.

Sasa huku ni kusimamia sheria au ni kuvunja sheria Mhe. Spika. Hivyo jamani tuone kwamba hii dunia tuliyo na hapa ndipo kwenye machumo ya huko akhera tunakokwenda. Mambo yote tunachuma hapa duniani tulipo, akhera hakuna tena kwamba unakwenda kufanya kazi nyengine upate thawabu kuweka pembeni. Unachuma hapa hapa duniani. (*Makofi*).

Sasa dhuluma kama hii inafanywa, na sisi tukawa tunaipapalia na kuifagilia, dhuluma haimalizi na dua ya mwenye kudhulumiwa Mtume (*S.A.W*) anasema kwamba haisimami mbingu zote zinapasuka anapoomba, anaponyanyua mikono yake akaomba kwamba anadhulumiwa, dua hii haisimami.

Sasa tujiulize kwa nini Zanzibar hatuendelei. Haya katika mambo ya dhuluma; kudhulumiana maendeleo katika nchi hii hayapatikani, kwa sababu hatupo tayari, kila siku tunadhulumiana, hata unajua kwamba haki kweli ni yake lakini unasababisha dhuluma, kitu kile muhusika asikipate, wapi tutaendelea.

Kazi yetu mimi ninasema itakuwa ni kuja kusifia nchi za watu tu kwamba wenzetu wapo hivi. Kuna watu tumewatangulia uhuru lakini kila kukicha sisi tunarudi chini tu, kwa sababu hatupo tayari. Haki za watu tunawanyima kwa makusudi kabisa, tutaendelea wapi. Lazima hatutoendelea.

Jamani tusione jua linakwenda, usiku unaingia. Tumo katika kufanya kazi na kazi hii mlipaji ni Mwenyezi Mungu, ukifanya dhuluma na wewe utadhulumiwa.

Mhe. Spika, naomba kwamba suala hili hawa watu ambao wameshatimiza sifa zao, vitambulisho bado kupewa tu, risiti wanazo, wameshapiga picha lakini hawajapewa vitambulisho, wengine wameshakwenda kwa Masheha wameshapata barua ile ya kwenda kupigishwa picha lakini hawapigishwi picha.

Wengine tayari vyeti wanavyo wako kwa Masheha, lakini Masheha hawataki kuwapa. Kumbe tulipopitisha hapa Sheria ya Maadili ya Viongozi wote wana CCM walisema kwamba Sheha atolewe, kumbe atolewe katika viongozi wa maadili, hatua moja ni hii, kwamba Sheha afanye anavyotaka na yeye ni kiongozi wa jamii.

Mhe. Spika: Muda wako umemalizika.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante Mhe. Spika. Kama ni hivyo Waheshimiwa basi ni lazima tuhakikishe kwamba Masheha hawa ambao hawafanyi wajibu wao basi wachukuliwe hatua.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma na kwa safu hii ya nyuma tumalizie na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ambaye anajitayarisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti hii ya Mhe. Hamad Masoud Hamad, mimi siiti hoja mimi ninaita ripoti.

Mhe. Spika, hii ninaita ripoti kwa sababu haina nguvu ya hoja. Haina nguvu ya hoja, kwa sababu na mimi nina hoja ya kuita kwamba haina hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi Mhe. Hamad Masoud Hamad ni rafiki yangu na yeye mwenyewe anajua, lakini leo hii taarifa yake, hii ameleta zaidi siasa kuliko hasa hoja.

Mhe. Spika, taarifa yake hii angeliileta katika kuchangia ripoti ya Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, pale ndiyo ilikuwa pahala pake. Lakini siyo kuleta kwamba ni hoja, sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na yeye mwenyewe kwa bahati nzuri ame-*quote* vizuri Katiba ya Zanzibar, kuna sheria zimetungwa. Sheria ambazo tulizozitunga sisi tuje tupate

shindikizo lake tuzikiuke, kitu kama hichi Mhe. Spika hatuwezi tukakikubali hata siku moja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ninatangulia kusema kwamba mimi ninaikataa na ninawashawishi wenzangu waikatae kwa sababu haina ushawishi wa kutushawishi tuikubali kama hoja kuiagiza Serikali ikavunje sheria tulizozitunga sisi Barazani. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninadhani Mhe. Hamad kwenye ukurasa wa mwanzo ameeleza vizuri kwamba Serikali imetengeneza Katiba, halafu imetengeneza na sheria. Lakini vile vile kuna vifungu alivyovi-*quote* Mhe. Hamad Masoud ile Sheria Na. 7, tatizo lake ali-*quote* sheria alishindwa kuangalia kwamba tulimlazimisha Waziri kutunga Kanuni, aangalie Kanuni Kifungu cha 13 (1).

Kifungu cha 13 (1) kinasema kwamba, "Mtu ambaye amekosa haki yake atakwenda kukata rufaa kwa Mkurugenzi". Lakini vile vile kama hakupata haki yake kwa Mkurugenzi mtu yule yule bado anayo nafasi ya kwenda kukata rufaa kwa Waziri, aangalie Kifungu cha 13 (2).

Je, leo niulize Mhe. Waziri yupo hapa, kuna rufaa gani aliyopelekewa na mwananchi aliyekosa haki yake. Sasa vitu hivi Mhe. Spika, watu wasije na ushabiki wao wa kisiasa kwa sababu mwaka 2015 imeshafika watu wanataka kura kwa kutumia mgongo wetu, haiwezekani! (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninataka niwaambie kwamba wenzetu sasa hivi wanatumia hoja kwa kufuta makosa yao. Kwa sababu kuna wakati waliwashawishi wananchi wasiende kuchukua vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na wakasema kitambulisho hichi hakina maana, mwisho Chumbe. Leo wanageuka wale wale wanakwenda kuiambia Serikali inawanyima vitambulisho.

Nataka nikwambie Mhe. Spika, jana Mhe. Subeit Khamis Faki nilimsikiliza sana, alisema kwa sauti kubwa sana na alisema kwa kuhamaki, kiasi ahamaki. Hawa wenzetu wametumia pesa nyingi kutengeneza vyeti feki, kila anayekuja hapa ana mabunda yake ya vyeti.

Mhe. Spika, mimi ninataka nikwambie juzi kwenye semina ulikuwepo, katika semina ile tuliambiwa sasa hivi kuna utaratibu wa *IT* wana-*scan*. Mhe. Spika, wanaweza waka-*scan* kichwa chako ikaingizwa na miguu yako na kama munataka mfano humu humu ndani ya Baraza tunatiliana tunarushiana mapicha, tusharushiwa mapicha kuna Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Pinda kavaa sijui rubega na nini wanacheza mziki, uongo?

Watu wana-*scan* pensi ya mtu mwengine wanabandika kichwa cha mtu mwengine. Mhe. Spika, kama munataka ushahidi mwengine aangalie matangazo ya TIGO. Joti anapomwita dereva, dereva! yule yule ndiye Joti, yule yule bosi ndiye Joti, lakini kuna tangazo jengine Joti yupo kondeni, Joti yule yule anamtuma bosi wake.(*Makofi*).

Sasa Mhe. Spika, Waheshimiwa hivyo vyeti ni vyeti feki. Tumeshawahi kuzungumza na Mkurugenzi wa Idara ya Vitambulisho.

Mhe. Spika, unaweza ukakiona cheti ni *original*, lakini cheti kile wameki-*scan* lakini unapo-*scan* kuna vitu unakuwa huvioni. Wenyewe wataalamu wameshavigundua, ndiyo maana

unapokwenda na orodha yako ya vyeti anakutizama tu, kuna vitu akiviangalia tu anajua cheti hichi kimeshatoka.

Jana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk katoa mfano mzuri. Kuna cheti kimoja wamepewa watu wawili. Kuna vitu vinaangaliwa. Sasa vitu hivyo sitaki kuvisema kwa sababu ili muendelee kula hasara, kutoa vyeti na mukienda mutakosa, munawakosesha watu haki zao. (*Makofi*).

Mhe.Spika, haya mambo ya ubabaishaji yameshatuathiri sana sisi Zanzibar. Mimi nitatoa mfano mmoja. Mhe. Spika, mwanzo mwanzo Wazanzibari sisi Watanzania tulikuwa sisi tunaingia Uingereza bila ya *visa*, lakini wenzetu walipofika wakati siasa wakatengeneza utaratibu wanafanya fujo, wanafanya nini, wanapiga picha wanarusha ili ionekane Zanzibar kuna fujo. Matokezeo yake Mhe. Spika, watu mimi ninao marafiki zangu walikuwa wanaambiwa unakwenda Mtendeni pale unakatizwa kadi ya CUF, kumbe ndiyo tiketi ya kwenda Uingereza mpaka leo wapo wengine wanashindwa kurudi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, leo imefika pahala Zanzibar tumeekewa vikwazo sasa hivi inabidi lazima tuingie Uingereza kwa *visa*, nchi za Jumuiya ya Madola kama Uingereza huingii kwa *visa*. Sasa Mhe. Spika, kuna watu wanajifanya wana akili nyingi lakini maarifa hawana. Kwa hivyo katika suala la vyeti, mimi ninawapongeza sana Masheha, mimi Mhe. Subeit Khamis Faki katika mikutano yako uliyokuwa unaifanya usiku usiku kwenye Jimbo la Kwamtipura, mimi niliambiwa na wananchi wangu, Sheha akaniambia Mhe. Subeit anafanya mikutano, wanaandaa utaratibu wa kuandalia watu vyeti.

Nikamwambia sikiliza Mhe. Subeit kazaliwa Micheweni, kakulia Micheweni, kaja mjini kwa kufanya kazi. Mimi nimezaliwa Chaani, nimekulia mjini, ninajua kila ujanja. Vimepelekwa vyeti alivyovipeleka Mhe. Subeit kuwapa watu wake, Sheha wangu wa Kwamtipura kavirudisha, ndiyo hivyo anavyolalamika navyo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, jana alipokuwa anachangia Mhe. Subeit nikatumiwa *message* ninayo nitakuonesha ukitaka, ninaambiwa huyo Mhe. Subeit aliyesema vyeti vyake ndivyo vile vyeti Mhe. Hamza tulivyokwambia anavitengeneza.

Sasa suala la vyeti Mhe. Spika, tusisakame Masheha, vyeti vyao kwa kweli ni feki na huwezi ukapata kitambulisho chochote cha Mzanzibari Mkaazi kwa ajili ya cheti feki. (*Makofi*).

Mhe. Spika, chengine kuna suala la kadhia iliyotokezea ya mkutano wa CUF. Mimi ninalaani...

Mhe. Spika: Una dakika 3.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sawa mimi ninalaani vitendo vile ambavyo vilivyofanyika, lakini ninalaani zaidi yule ambaye amenihusisha mimi na matukio yale yaliyotokezea kule.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa katika mkutano wa Kiembesamaki kwenye mkutano wetu wa chama, wenzetu walikuwepo Makunduchi. Vijana wangu wa Jimbo la Kwamtipura, mimi hawakupanda Fuso, wamepanda mabasi, siku hizi Kwamtipura hatupandi Fuso tunapanda basi.

Basi zilikuja pale watu wanang'ara. Leo ninakuja kuambiwa aah! vijana wa Mhe. Hamza wamepiga watu. Mhe. Spika. Ni lazima tuwe wakweli, haya mambo ya chuki hayatusaidii, siyo wakati wake.(*Makofi*).

Lakini cha mwisho Mhe. Spika, kwa wale wenye ndoto za mchana ya kusema kwamba watashinda uchaguzi. Mhe. Spika, Chama cha Mapinduzi sisi tunakwenda kwa takwimu, na nyinyi kama mulikuwa munategemea ushindi kwa vyeti basi imekula kwenu. Kitu ambacho ninachokwambia sisi CCM tutarudi madarakani na tutaendelea kuongoza nchi hii na kama tulivyosema mwanzo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, hoja hii ninamalizia. Hoja mimi ninaichana, hii si hoja, hii wala si hoja, wala haina maana ya kuitwa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ninamalizia dakika yangu moja, umeniambia tatu, imebakia moja. Mhe. Spika, hoja kama hii tuliwahi kufanyiwa sisi mwaka 2010 alipokuja na hoja Mhe. Abubakar Khamis Bakary, hoja ya kukubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sisi tulikataa na Mheshimiwa wewe shahidi. Dkt. Karume akatwambia ikubalini, tukamwambia itakuwaje hoja. Kama ni hoja ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni hoja ya Chama cha Mapinduzi alete mpinzani, akasema chonde chonde ikubalini.

Mhe. Spika, tukaikubali hoja ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Leo yanayofanyika kweli ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kila siku viongozi wetu wanatukwanwa, kila siku mashaka juu ya mashaka. Tulipitisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili kuondoa maovu, unyanyasaji. Shekhe Soroga yule pale, wamemtia *acid*. Kwa hivyo Mhe. Spika, kama mulitupata wakati ule kukubali hoja, sasa hivi hamtupati tena, tumeshaamka. (*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya hayo machache hii hoja naomba isiungwe mkono, haina maana wala haina maana hata kidogo, na kama mulikuwa munategemea mtashinda kwa sababu mumempata Mhe. Mansoor Yussuf Himid, Mhe. Spika, Mhe. Mansoor Yussuf wameshampata, lakini ushindi hampati.

Ahsante sana Mhe. Spika, siungi mkono hii hoja. *(Makofi/Vicheko)*

TAARIFA

Mhe. Spika: Taarifa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Samahani Mhe. Spika, mimi sisemi mtu gani, nasema tunahitaji kusikia maoni yanayotolewa. Sasa Mhe. Hamza Hassan hatukumsikia kasema nini.

Mhe. Spika: Ni kweli, haya nimesikia. Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli kwamba kama tukipiga makofi sana haidhuru kwenye Hansard yanaingia, lakini mtoa hoja baadaye tutamwita tutamtaka ajibu na hakusikia kitu. Sasa ni vizuri kama kuna jambo limefurahisha tukapiga makofi lakini kwa nidhamu, ili kumpa nafasi anayechangia asikike na mtoa hoja apate kusikia na sisi Wajumbe tuweze kusikia, kwa sababu kuna wengine wanaweza wakasema kwamba mimi sina zaidi naunga mkono aliyosema mwenzangu itakuwa imekwisha na ametuokolea muda.

Lakini mwengine anaweza kusema mimi naomba kutofautiana na aliyesema fulani. Sasa kama hakusikia maana yake inabakia kwenye Hansard, lakini mualo wa majadiliano humu ndani itakuwa sio mzuri, tunaweza tukapiga makofi lakini kwa nidhamu.

Haya tuendelee basi kwa kumsikiliza Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kabla hatujaenda kwenye safu ya mbele.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena kupata fursa ya kusimama na mimi nikazungumza mawili au matatu. Lakini kisimamo cha sasa hivi Mhe. Spika, nakuja katika kuchangia kwenye hii hoja ambayo imewasilishwa na jirani yangu hapa Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu niende moja kwa moja katika mada ambayo iko mbele yetu. Mhe. Spika, nilijaribu kutafuta Hansard ambayo ilikuwa imehalalisha uanzishwaji wa sheria ya vitambulisho. Katika Hansard hii ya tarehe 11 Aprili, 2005. Mhe. Spika, kuna mambo humu mazito kweli.

Mhe. Spika, nilikuwa najaribu kuangalia hususan michango ya Mhe. Ali Rashid Ame Mwakilishi wa Jimbo la Ole, Mhe. Haji Faki Shaali na Mhe. Salim Hamad Saleh. Maelezo ambayo yamo katika Hansard hii, nikioanisha na leo Mwakilishi wa Jimbo la Ole ndiye amekuja kuleta hoja hii hapa, kwa ajili ya kuja kujadiliwa ni vitu ambavyo kidogo vinanipa mashaka.

Mhe. Spika: Mhe. Subeit Khamis Faki na Mhe. Shadya Mohammed Suleiman tumsikilize anayechangia.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Lakini nikiondoka hapo Mhe. Spika, nakuja sasa katika hoja yenyewe.

Mhe. Spika, katika hii hoja ambayo imeletwa hapa, mleta hoja ameizungumza Katiba ya Zanzibar kifungu cha 6(1), naomba nikariri kwa ruhusa yako. Kifungu hiki Mhe. Spika, kinasema kwamba;

Kifungu 6(1)

> "kutakuwa na Mzanzibari ambaye upoteaji wake na urudishwaji wake, utakuwa kama ilivyoainishwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi",

Ili niweze kufahamika Mhe. Spika, naomba pia unipe fursa ya kusoma kifungu cha 5(a) cha Katiba ya Zanzibar. Kifungu hiki kinasema hivi;

Kifungu cha 5(a)

> "Zanzibar inafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu;

(1) Mamlaka ya Utendaji, Mamlaka ya Kutunga Sheria, Mamlaka ya Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma, na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki.

(2) Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya Utoaji Haki ni Mahakama".

Maeneo haya matatu Mhe. Spika, nikishayasoma, sasa nikija kuangalia sasa uhalisia, kazi ambayo imekwishafanywa na Baraza la Wawakilishi, ikiwa ni kazi yake kutunga hiyo sheria. Sasa kusimamia haki sasa na masuala mengine, haya masuala sio tena ya Baraza la Wawakilishi, kwa mujibu wa taratibu zetu Mhe. Spika, tulizojiwekea, kazi ya kusimamia haki ni kazi ya Mahakama.

Kama kuna mtu alikuwa anatafuta haki yake katika utaratibu huu wa sheria ambazo tunazitunga hapa, kazi hii Mhe. Spika, nataka nifahamike kwamba ni kazi ambayo inasimamiwa na mahakama.

Baraza la Wawakilishi, katika suala zima la kutengeneza hoja ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, imetengeneza sheria namba 7 mwaka 2005, kwa hivyo jukumu la Baraza hili sasa kuzungumzia suala hili limeishia pale. Sasa nikiangalia katika utaratibu, katika utafiti ambao nilikuwa nimeshaufanya, inapokuwa kuna matatizo kwa mujibu wa sheria wenzangu walikwishafahamisha kama ambavyo walikariri zile sheria mbali mbali ambazo wamezizungumza hapa.

Lakini ukiangalia Mhe. Spika, tuangalie sasa katika ile fursa ya watu ambao wamekoseshwa hivyo vitambulisho na wajibu wao ni nini wafanye.

Mhe. Spika, kwa utafiti mdogo ambao nimeufanya, watu ambao watakuwa wamekoseshwa haki hiyo, wanatakiwa wafuate taratibu za kisheria likiwemo suala la kwenda kukata rufaa katika mamlaka husika.

Mhe. Spika, katika taarifa za utafiti ambao nimeufanya ziko rufaa ambazo zilikatwa katika miaka ya 2010, 2011, 2012, 2013 na mwisho kumalizia katika mwaka 2014. Baada ya mwaka 2014 Mhe. Spika, hakuna rufaa yoyote ambayo imewasilishwa katika kitengo, cha kuwa kuna watu ambao wamelalamikia suala la kitambulisho chao ambayo ipo kwa Mkurugenzi. Sasa leo hoja inapotoka ikaletwa hapa ina maana gani Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba sana kazi hizi tunapozifanya tuangalie taratibu za kisheria, tusiende tu katika masuala ya kishabiki na hatimaye kuweza kusababisha vitu ambavyo havikutarajiwa kutokea katika maeneo yao.

Mhe. Spika, vile vile nilifanya kazi ya kufanyia utafiti utaratibu wa vitambulisho ambavyo vimeweza kutolewa katika wilaya 10, je, inakwenda sambamba na kwamba kuna watu wanakosa vitambulisho.

Mhe. Spika, kwa utafiti ambao nimeufanya, nimegundua kwamba kuna vitambulisho vingi sana vimeweza kutoka katika maeneo husika kwa wilaya zote 10 ndani ya Zanzibar yetu. Sasa nikiangalia vitambulisho ambavyo vimetoka Mhe. Spika, na nikiangalia takwimu za *population* ya watu wa Zanzibar ni vitu ambavyo kidogo mimi vinanipa mashaka. *ZAN- ID* ambazo

zimekwishatoka mpaka sasa ni 651,899, ukiangalia *population* ya watu wa Zanzibar ni milioni 1.3. *Age* ambayo inakubalika kupewa hivi vitambulisho ni kuanzia miaka 18 Mhe. Spika, lakini ukiangalia *average* ya watu ambao wanapatiwa hivi vitambulisho vyenyewe ni kati ya asilimia 47 na 50. Sasa laki 651,899 ukiigawa kwa *population* ya Zanzibar milioni *1.3 times 100 percent* tunapata *50. 15 percent* ya watu ambao tayari wameshapata vitambulisho. Sasa tuangalie na wapiga kura wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba mtoa hoja yake atakapokuja hapa anisaidie katika mahesabu haya, ili na mimi niweze kufahamu vizuri jinsi ya huu utoaji wa vitambulisho unavyokwenda katika maeneo yetu. Mimi napenda sana kuangalia masuala ya mahesabu na manambari haya kama ambavyo Mhe. Hamza Hassan amezungumza. Suala la takwimu ni muhimu.

Mhe. Spika: Una dakika tatu. bado dakika tatu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Jengine la mwisho ambalo nataka kulichangia Mhe. Spika. Kuna Mjumbe mmoja alikuja kuchangia hapa na akawagusa jamaa zangu wa Kimakonde. Mzee wangu hapa, kuna mwenzangu alimpa cheo cha kumwita muasisi katika nchi hii na katika Baraza letu hili. Lakini sasa kutokana na kile kitendo cha kushangazwa na Wamakonde kupewa vitambulisho katika nchi hii.

Kwanza Mhe. Spika, nataka ni-*declare interest* hapa. Ubalozi wa Msumbiji Zanzibar umo ndani ya Jimbo la Kikwajuni, ni swahibu zangu na wako karibu pale. Sasa vinapotokezea vitu kama hivi sisi wengine huwa tunaathirika kidogo. Katika Mapinduzi ya nchi hii Mhe. Spika, nimeyasoma na naendelea kuyatafuta kwa sababu kazi yangu ni utafiti mimi.

Katika historia ya nchi hii Mhe. Spika, Wamakonde wamecheza nafasi kubwa sana katika kuhakikisha kwamba Mapinduzi ya Zanzibar yanafanikiwa tarehe 12 Januari, 1964. Unapofika ukasema kwamba kuna ubora gani wa kuweza kupewa mtu wa Kimakonde kitambulisho. Nataka ifahamike bayana kwamba Wamakonde kwa kazi waliyoifanya kwenye nchi hii basi wanaweza kuwa na nafasi kubwa zaidi, kuliko hata yule aliyesema kwamba kwa nini wamepewa wao kwa mujibu wa historia.

Mhe. Spika, kwa kumalizia. Kuna Mjumbe mwengine alizungumzia suala la vitambulisho katika jimbo lake, kwamba vitambulisho kuna watu karibu 30,000 hawajapata.

Mhe. Spika, kwa takwimu ambazo nimekwenda kuzitafuta, kwa majimbo yote 50, hakuna jimbo hata moja ambalo lina vitambulisho zaidi ya 22,398, kwa mujibu wa takwimu ambazo zipo katika taasisi inayoshughulika na vitambulisho. Kwa msingi huo, na kwa maelezo haya ambayo nimeyatamka hapa Mhe. Spika, hoja hii haina mashiko, hoja hii haijitoshelezi na hoja hii siiungi mkono.

Naomba kuwasilisha Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Sasa ni wakati muafaka kwa safu ya mbele. Katika safu ya mbele hii tunaanza na waombaji ambao ni Naibu Mawaziri. Nichukue nafasi hii basi kumkaribisha Mhe.

Mtumwa Kheir Mbarak; Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili. Baadaye Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kufika katika Baraza hili ili kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwanza kabla ya kuanza kuchangia hoja hii, mimi niseme naiunga mkono hoja hii. Unapounga mkono kitu bila shaka una sababu zako.

Kwanza nimpongeze Mhe. Hamad Masoud Hamad. Kuna kitabu kimoja kinaitwa Taalim, kitabu hiki kinasema mwanamme aliyekamilika anakuwa na mambo mawili.

Kwanza ana ushauri, bila shaka Mhe. Hamad Masoud alitafuta ushauri juu ya kadhia hii iliyokuwepo katika nchi yetu. Halafu anakuwa na rai kwenye kusibu, kwa hivyo baada ya kupata ushauri akatafuta na rai ili kuweza kuleta hoja hii ipatiwe ufumbuzi. Kwa hivyo, na hili mimi nampongeza.

Mhe. Spika, tangu jana kulikuwa kuna mjadala mrefu juu ya hoja hii. Kuna waliosoma sheria hapa, wakatoa sheria zao juu ya hili, kuna wengine waliopotosha sheria, yote hayo jana tulisikiliza mijadala iliyotokea. Lakini mimi ningeomba kuuliza kitu kimoja Mhe. Spika. Kitambulisho ni haki ya mtu au sio haki ya mtu, tukishajua kwamba kitambulisho ni haki ya mtu au sio haki ya mtu. Kama ni haki ya mtu, kwa hivyo utaratibu kwa hawa ambao hawana vitambulisho na utafutwe uchunguzi wa kutosha, wa kwamba hawa hawana na ni sababu gani wakawa hawana, ili wapewe haki yao.

Mimi sioni sababu wala sioni shida kumuona mkwe wangu hapa kuichana hii ripoti, sioni shida, kuna watu wanachana msahafu, wanauchana msahafu Mhe. Spika, kwa sababu aya za Mwenyezi Mungu zinazosema zikimgusa yeye hazitaki, ana hakika Mwenyezi Mungu kasema ndani ya Qur-ani *Walaa Taqrabu Zinaa* na kuiacha hataki*, Walaa Taqrabu Dhulma* na kuiacha hataki, sasa asichane msahafu, hakubaliani na zile sharti za Mwenyezi Mungu, sasa mimi sioni ajabu leo mkwe wangu kuchana hii ripoti, sioni ajabu wala sioni shida. Lakini ajue kama *Man tabaa qaumun fahuwaminhum*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ikiwa haki ya kitambulisho kila mmoja ana haki ya kupatiwa, na kila mmoja suala hili limemgusa katika wilaya yake au katika jimbo lake, limetugusa. Malalamiko yako mengi, lisemwalo liko halizushwi. Kama cheti *fake* kimetolewa na nani?

Mimi leo naondoka nyumbani kuna cheti cha mjukuu wangu ambaye kazaliwa juzi, anaitwa Jamal Seif Ali, naondoka ananiambia mama chukua cheti changu kimeandikwa Jumali, kaandika nani, anafika kule shilingi 15,000 kubadilisha cheti kile, nani kaandika na wamepelekewa jina Jamal Seif Ali, naambiwa shilingi 15,000 kubadilisha hapo, kaandika nani? *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hivi ni vitu vya kuvitizama na siku zote kama mtu haki yake Mtume anasema hivi *Alhaqqu ya'aluu!* haki siku zote kazi yake kupanda juu, *Walaa yu'ula alayhi* wala haipandiwi juu yake, itatoboa.

Kwa hivyo, mimi naiomba serikali kwa kuwa mara nyingi vidole huoneshewa serikali, na wakati serikali inaoneshewa vidole, hebu tuondokane na kundi hili la dhulma. Nashauri tuondokane na kundi hili la dhulma, tufanye uchunguzi watu waliokuwa hawana vitambulisho wapewe kwa sababu hii ni haki yao.

Siku moja Mhe. Spika, nilikuwa naangalia kaseti fulani katika msikiti fulani kulikuwa na Sheikh anatoa mawaidha. Yule Sheikh akawa anasema siku utakayomuona dhalimu anauma kidole, basi pana mkubwa mmoja mara kahangaika mguu hivi, mara machozi yanamtoka analia, mara katikisa mguu hivi anataka atoke pale kwenye msikiti hawezi, anaona ile aya tayari imeingia kwenye mifupa na kwenye maini.

Kwa hivyo, tunaposomewa aya za Mwenyezi Mungu tunakuwa tuna hofu pale pale lakini tukiondoka basi. Kwa hivyo, hii ni dhulma jamani, kumnyima mtu haki yake na dhulma hii itatupelekea pabaya, na wakati dhulma hii tunaiona wazi wazi na tunaifurahia na kuishangilia.

Kwa hivyo, mimi nashauri serikali kwa hili, serikali ifanye uchunguzi, tusiingie kwenye siasa, tukiingia kwenye siasa hatufiki tunakokwenda, hatufiki. *(Makofi)*

Firauni alikuwa na urefu sentimita 75 tu, ndevu zake mpaka miguuni na akajinata akajinasibu akazaliwa mtoto wa kiume anachinja, kwa rehema za Mungu kaja kamlea Sayyidna Mussa, Sayyidna Mussa alipomlea ndio sababu ya Firauni kuja kupinduliwa ufalme wake, kwa hivyo halishindwi kwa Mwenyezi Mungu jambo lolote, Mungu hashindwi na chochote, Mungu hafundishwi.

Mhe. Spika: Una dakika tatu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Kwa hivyo namuomba Mwenyezi Mungu kwamba atujaalie Serikali tuone kuna kadhia kubwa ya watu ambao hawajapata vitambulisho, na vitambulisho hivi ni haki yao, na kama ni haki yao wapewe, laa wanaona si haki yao basi. Kwa hivyo mimi nadhani nilikuwa sina mchangio mwingi, ilikuwa nikazie hilo tu nakushukuru.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ingawaje na mimi nina mchango mdogo tu sina mchango mkubwa sana, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu *subhanahu wataala* kwa kutuwezesha kuwepo hapa asubuhi hii tukiwa wazima wa afya na salama na amani.

Lakini kabla ya kusema lolote naomba na mimi niunge mkono hoja ya Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa asilimia mia moja. Naamini kwamba Mheshimiwa Hamad kaileta hoja hii ilhali ya kuwa tayari ishafanyakazi, ishapita kwa wananchi na ishaujua ukweli, kwa hivyo niseme kwamba ukweli utabaki kuwa ni ukweli. Na uongo hata kama utaujenga katika hali gani ili uufanye uwe ukweli basi uongo utabakia katika hali yake ya uongo.

Nimuombe Mhe. Waziri husika wa vitambulisho kaka yangu Mtumbatu mwenzangu nimuombe sana kwamba ajaribu kulifuatilia suala hili ipasavyo ili ajue ukweli, kwa sababu ukweli uko wazi

kwamba wananchi wengi wananyimwa haki yao ya vitambulisho, hili nalizungumza nikiwa na mimi nina ushahidi wa kutosha, hususan nizungumzie jimbo langu la Nungwi, suala hili hili la wananchi kunyimwa vitambulisho wakati Wizara hii anaisimamia Mhe. Mwinyihaji nashukuru kwamba suala hili alilichukua vizuri, na nathubutu kusema kwamba kalifuatilia namshukuru sana Waziri, kalifuatilia na akamleta Mhe. Mkuu wa Wilaya ndani ya Nungwi, wakajikusanya wananchi wakapeleka vyeti vyao.

Mhe. Mkuu wa Wilaya alichokitaka kwamba wananchi wale siku ya pili wamfuate ofisini kwake Gamba, nashukuru kwamba wananchi wale wamefika ofisini kwake Gamba pamoja na vyeti vile, lakini cha kusikitisha zaidi baada ya kufika Gamba Mhe. Mkuu wa Wilaya kakataa, akasema vyeti vile vyote feki. Jambo la kusikitisha lazima tukubali ukweli.

Mhe. Waziri alifuatilie suala hili ajue ukweli wa watendaji wetu wasiwadanganye watu, tulifuatilie tupate uhakika. Isitoshe mimi mwenyewe, mtoto wangu mwenyewe, niliyemzaa mimi mwenyewe, Mwadini Haji Mwadini wakati anatafuta kitambulisho kaenda katika Wilaya ya Kaskazini(A) mara tatu na cheti chake cha kuzaliwa kila anapofika Wilayani anaambiwa kwamba cheti chako feki, mke wangu akanipa taarifa kuna siku nikatoka naye mimi mwenyewe tukaenda katika Afisi ya Vitambulisho Kaskazini, baada ya kufika wapo pale maafisa kina Mzee Ali na wengine.

Lakini baada ya kufika mimi, baada tu ya kuona kile cheti wakasema kweli Mheshimiwa kulikuwa na makosa tu madogo madogo lakini ilikuwa hatujakaa, siku ile ile kapigwa picha na sasa hivi kitambulisho anacho. Jamani cha kujiuliza zaidi huyu mtoto wangu kapata kitambulisho kwa sababu ya kwenda mimi mwenyewe, kuna watoto wangapi wa watu ambao si viongozi wa nchi hii ambao wanakoseshwa vitambulisho. Ukweli utabakia kuwa ukweli, naomba sana jamani tujiwekeni sawa tufuatilie haya masuala ikisha tutafute njia ya kuwasaidia wananchi, bila ya hivyo tutafikia pahali pabaya. Mimi naomba sana viongozi wenzangu hili suala tulifuatilie.

Lakini la mwisho la kumalizia mimi nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kasifu sana, kafanya takwimu za ushindi wa chama, na nilikuwa sifikirii kama tutayazungumzia hayo kwa sasa hivi, lakini kadri ya alivyosifu na akasema kwamba ana uhakika wa kushinda Chama cha Mapinduzi hiyo ni siri ya Mungu, wakati ukifika hakuna hata mmoja anayeweza kupambana na wakati wala kuzuia wakati hilo likubalike. Sasa yeye kathibitisha hapo kwamba Chama cha Mapinduzi kitashinda, kitaendelea kushinda na mimi mwanachama wa CUF nasema CUF itashinda na itaongoza nchi hii.

Ndiyo yeye kasema kisiasa na mimi nasema hivyo hivyo, kwa hivyo Mwenyezi Mungu anajua kila kitu, ndiye mpangaji wa yote. Mwenzangu kazungumza hapa kwamba ulikuweko utawala wa Firauni hakuna utawala uliokuwa mgumu kama huo lakini kaondoka, kwa hivyo haya yote ni mipango ya *Allah subhanahu wataala*.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana *(Makofi)*

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum na MBM) Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuzungumza machache sana kwa siku ya leo. Mimi

Mheshimiwa nasaha zangu ninazotaka kusema kwa wenzangu kwamba umoja haujengwi kwa matofali, umoja hujengwa kwa misingi yake maalum. Lakini ingekuwa umoja hujengwa kwa matofali Mheshimiwa Spika, wala mimi nisingesimama nikasema chochote leo, lakini nimegundua kwamba Mhe. Spika, kwamba huwezi kujenga umoja kwa kutumia matofali, umoja unajengwa kwa misingi maalum.

Mhe. Spika, misingi ya kujenga umoja kwanza ni kuwa na haki katika nchi. Kuhakikisha kwamba raia wote unawapa haki sawa, lakini ukiwa na raia ukaanza kuwagawa mapande; kundi moja ukalipa haki kundi moja ukalinyima haki hapo unakuwa unabomoa misingi ya umoja. Sasa hata ukihubiri katika majukwaa umoja umoja lakini kama *practice* inayofanywa sio ya kujenga umoja Mhe. Spika, umoja huo utakuwa si umoja wa kweli.

Sasa Mhe. Spika, mimi ombi langu na sisi wanasiasa tuiache hii ofisi ya vitambulisho iwe huru, ifanye mambo yake bila ya kuingiliwa. Sasa hivi Mhe. Spika, kwa kweli tumeiingilia sana hiyo ofisi ya vitambulisho, na kwa kweli kinachofanywa ni siasa si jambo jengine.

Mimi Mhe. Spika, nataka niwasifu sana Masheha wa Jimbo langu la Mkanyageni walijaribu kuwanyima watu fomu, lakini kidogo kutia nguvu zangu wakaheshimu wote wananchi wamepewa fomu, lakini sasa tatizo fomu wamepewa wamekwenda ofisi za vitambulisho wamepigwa picha wamepewa risiti lakini vitambulisho wanaambiwa mpaka ipite kuboresha daftari ndio wapewe vitambulisho vyao.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukiwaambia watu mpaka daftari liboreshwe ndio wapewe vitambulisho vyao mnakusudia nini, kwa sababu wale wanataka vitambulisho vyao wakajisajili katika daftari la wapiga kura, leo wanakwenda wanaambiwa musubiri mpaka daftari lipite halafu mtapewa vitambulisho vyenu, kwa maana hiyo Mhe. Spika, hii ofisi tunaitumia vibaya.

Na mimi suala langu ninaloliuliza hawa wafanyakazi wanasusia vitambulisho na sisi wanasiasa ambao tumeteuliwa na Rais kumsaidia kazi, ndio kweli tunamsaidia Rais kazi, hivi mimi imani yangu kwamba hatumsaidii Rais, kwa sababu kama Rais kala kiapo cha kuwatumikia wananchi wote, sasa ikiwa sisi tunaitumia ofisi hii kuwanyima watu wengine haki na kuwapa watu wengine haki ina maana hatumsaidii Mhe. Rais, kwa hivyo mimi ndio wito wangu kwamba sote tulioteuliwa na Mhe. Rais basi kwa uaminifu kabisa tumsaidie Mhe. Rais majukumu yake vilivyo bila ya kutukuza ushabiki.

Mhe. Spika, mimi nataka nitamke wazi kabisa kwamba mimi Mhe. Haji Faki Shaali hata siku moja bilisi hatonisogelea kutaka umoja wa Wazanzibari upotee, maana kuna watu wanashangilia sana sasa hivi wanasema hatutaki serikali ya umoja wa kitaifa, hatutaki hichi hatutaki hichi, lakini Mhe. Spika, mimi narudia nyuma tulikotoka wewe umetumika Wete siku ngapi tukaja tukazungumza tukakataa kuja katika Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli tunatoka mbali Mhe. Spika, tulikuwa katika mizozo hatuvutani hatushirikiani, leo Mwenyezi Mungu *inshaallah* katujaalia tumejenga umoja, leo umoja tunataka kuuvunja kwa vitambulisho Mhe. Spika.

Kwa hivyo mimi Mhe. Spika, ushauri wangu kwamba watu wote wapewe vitambulisho vyao, wale masheha waliowanyima watu fomu wawape hii ni haki yao, kama chama cha siasa kila

chama kitafute mbinu za kupatia ushindi lakini tusitafute ushindi kwa kutumia ofisi ya vitambulisho. Nakushukuru Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said(Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum na MBM): Mhe. Spika, awali ya yote nianze kukushukuru lakini pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama leo na mimi nitoe mchango wangu katika hoja hii binafsi iliyoletwa na Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Spika, awali ya yote niseme kwamba nimewasikiliza Wajumbe karibu ya wote wakichangia mada hii, lakini wengi au karibu wote tunasema hoja hii haina fani ya kisiasa, lakini tunazungumza kisiasa, sasa bora tukubaliane hoja hii imekuja Barazani kisiasa kwa ajili ya siasa, na kwa sababu imekuja kisiasa mimi siungi mkono hoja hii.

Kwa nini nasema siungi mkono, nafikiri Mhe. Haji Faki Shaali kazungumza vizuri Idara hii ya Mrajis wa Mzanzibari Mkaazi inafanya shughuli zake kama kawaida na kwa ufanisi mkubwa, sasa tunapoleta hoja ina maana haturidhiki na utendaji wa idara hii, mimi naridhika nayo na wanafanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, mimi nafikiri shida yetu kubwa ni kutafsiri nusu ya neno lenyewe kweli sote ni Wazanzibari lakini vitambulisho hivi sio Wazanzibari tu ni vya Wazanzibari wakaazi, kwa hivyo unaweza kuwa Mzanzibari lakini Mzanzibari wenyewe unaishi Donge, kwa hivyo kitambulisho chako upewe Donge, haiwezekani unaishi Donge useme kitambulisho upewe Mwembemakumbi hilo ndio naona tatizo kubwa liko hapo. Kama tutakubaliana kwamba kila mmoja apate kitambulisho katika eneo lake analoishi kwa uhalali nafikiri hizi hoja tukapeleka mpaka kwa Mungu maana yake tumeambiwa watu dhulma, serikali dhulma, tunadhulumu nini na wakati mwengine mtu yuko Serikali hiyo hiyo lakini anasema Serikali yenyewe dhulma, sasa kwa kawaida ukiwa na serikali dhulma na wewe uko Serikalini unatakiwa utoke usifanye dhulma.

Mhe. Spika, mtu anakuja anasema kaenda mazikoni Mwakilishi huyo jimbo lake sio lake, kufika huko mazikoni akakusanyiwa vyeti huoni hilo kama ni jambo la ajabu, kwamba wewe Jimbo lako Chambani umekwenda mazikoni Mtopepo umefika Mtopepo unapewa vyeti hajaandikishwa haya yalikuwa maziko kweli hayo au maziko ya kutafuta vyeti, maana hilo eneo lenyewe alilolisema huko Mtopepo pia kuna hizo habari za kuandikishwa vyeti bandia.

Na Mhe. Spika tusikatae kuna maeneo maalum, huwezi kwenda Mkoa wa Kusini ukaambiwa watu wanalalamika vyeti, lakini hata mjini sio sana lakini Wilaya ya Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Unguja ndio shida kubwa ilipo na kuna maeneo kama magharibi, ukianza Kisauni, Tomondo, Mwanakwerekwe, ukienda Magogoni, Kinuni halafu uje Mtoni, Bububu, Mwanyanya, Kihinani na kwa Wilaya ya Mjini Mpendae, Kwamtipura, Magomeni na sehemu ya Chumbuni hayo ni maeneo maalum.

Mhe. Spika, na kwa nini tujiulize kwa nini maeneo haya tu yawe hivi, kwa nini mfano mimi jimbo langu Mwembe Makumbi hakuna tatizo hili kwa sababu pale hakuna wakaazi wageni wahamiaji, lakini ukienda Shehia ya Chumbuni watu wanaokuja kujiandikisha wanavuka barabaraba wanakuja Chumbuni, Kwamtipura halikadhalika Kilimahewa

Kwa hivyo mimi ningeliwaomba ndugu zetu wanaotaka hoja hii bora wangeliwatafuta hawa watu wakawaambia warudi kwenye maeneo ya asili walipokuwa wanaishi wakajiandikishe wapate vyeti vya Mzanzibari mkaazi, kuliko kumuondoa mtu katika eneo lake kwa kumtuma aende eneo jipya akajiandikishe kwa sababu ya uchaguzi tutawakosesha haki kama mnavyozungumza. Lakini mimi nina hakika kama mtu yeyote atakuwa katika eneo lake husika hawezi kukosa haki yake ya msingi, mimi nina mtoto wangu anakaa Michenzani lakini alikuwa kajiandikisha Mwembemakumbi kahamia Michenzani, hakuweza kuhamia kule kwa sababu muda ulikuwa bado mpaka sasa umetimia ndio anahamishia uhamisho wake.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hapa tutazungumza sana hapa, tutazungumza kwa kelele lakini kama hatukuitafsiri vizuri sheria, na kwa bahati nzuri sheria hii inaambatana sana na sheria ya Uzanzibari.

Juzi Mhe. Spika tulikuwa na semina tukaulizana hivi unaweza kuwa Mzanzibari bila ya kuwa Mtanzania, wengine wanasema wao si Watanzania lakini ni Wazanzibari, mimi nikasema haiwezekani lakini watu wanasema hivyo. Lakini najua ule ni utashi wa kisiasa lakini sheria ya Mzanzibari ndio ambayo pia inatoa haki kwa sheria hii nyengine ya vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi, maana kuna sheria ya Mzanzibari halafu kuna sheria ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Kwa hivyo jambo hili linaweza kutatuka kama watu wote watarejea katika maeneo yao, ukivamia hata ukikaa miaka kumi kwa sababu umekuja hukuripoti kwa sheha, hujulikani unafanya kazi gani, wewe pengine unaingia saa saba za usiku unalala, alfajiri saa kumi na moja unatoka, hivi kweli utakuwa raia wa eneo hilo kweli, haiwezekani. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi kwa ufupi nimesema hayo nakubaliana na mwenzangu kwamba tusizungumze kwa jazba, hii ni taasisi ya Serikali inafanya kazi nzuri lakini isipewe mashindikizo.

Mhe. Spika, nimalizie mimi siku moja nilikutana na kijana anasema kapoteza kitambulisho chake cha Mzanzibari Mkaazi, akaulizwa na wahusika hicho kitambulisho ulikipatia wapi akasema nilikipatia Micheweni. Sasa umekipoteza unataka upewe cha wapi, nipewe cha Chumbuni. Mimi nikamuuliza wewe Chumbuni unakaa sehemu gani katika panga panga akasema anakaa kwa fulani, sheha wako nani anamjua sheha fulani, nikamuuliza watu wawili maarufu wa pale mtaani hamjui hata mmoja, nikajua huyu sio mkaazi isipokuwa kaelekezwa kufanya hivyo na nilikuwa na wasi wasi kama hicho kitambulisho kweli kimepotea. Sasa ni ujanja wa aina nyingi.

Mhe. Spika, namalizia kusema kwamba kila mtu arejee katika eneo lake akaandikishe, nina hakika hakuna ambaye atanyang'anywa. Mimi nishawahi kukutana na ndugu zangu wa Micheweni Kenya, wako Kenya lakini wanavyo vitambulisho vya Mzanzibari sasa fikiria wewe Kenya Malindi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema hoja hii mimi siungi mkono, tuache taratibu za kawaida, tuache Serikali ifanye kazi zake.*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naomba nianze kwa kutoa pole kwa Wazanzibari, ndugu zetu na wanachama wa Chama cha Wananchi *CUF* ambao wamepatwa na mtihani wa kujeruhiwa kwa kupigwa na

kuumizwa afya zao. Nimuombe Mwenyezi Mungu awajaalie afya. Lakini niiyombe vile vile serikali ilichunguze suala hili na kuchukua hatua zipasavyo, ili kukomesha vitendo vya kiharamia vya aina hii, ili nchi yetu ibakie katika amani na utulivu.

Mhe. Spika, nimelazimika kusimama kama Mserekali na mimi naomba nianze kusema kwamba mimi naiyunga mkono hoja hii. Kwa nini naiyunga mkono. Ni kwa sababu baada ya kuisoma na kuona mapendekezo ambayo yapo mimi sioni ugumu wa utekelezaji wa haya ambayo yameagizwa humu kwa serikali. Ningeshauri sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu tuungane pamoja ili suala hili tuliweke vyema.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna matatizo, matatizo yanazungumzwa Mhe. Spika, wee ni shahidi na wengine wote ambao wanaliongoza Baraza hili akiwemo Naibu Spika, na Wenyeviti. Wakati wote linapotokea suala linalohusu vitambulisho vya Mzanzibari au wakati wa bajeti humu ndani ya Baraza lako huwa hapatoshi. Na si hapatoshi kwa sababu tu Wajumbe wanapenda kusema na kulalamika, lakini lina ukweli ndani yake.

Mhe. Spika, mimi niombe sana, tunachopigania kelele humu na wengine kuikataa hoja hii mimi nakuwa sikifahamu. Kwa sababu kinachosemwa humu ni kuwapatia haki zao wale ambao wananyimwa haki zao kwa mujibu wa sheria, kwa mujibu wa Katiba na Sheria yenyewe ya Vitambulisho na Sheria ya Mzanzibari ambayo tumeitunga ndani ya Baraza hili.

Mhe. Spika, hakusemwi ndani ya hoja hii kuwapa vitambulisho ambao sio wakaazi wa maeneo. Hakuzungumzwi ndani ya hoja hii kuwapa vitambulisho watu ambao wana vyeti feki vya kuzaliwa. Kinachozungumzwa humu kwamba kuna tatizo pengine inawezekana sana kwamba baadhi ya Masheha kwa ajili tu ya utashi wao binafsi wanalikoroga jambo hili.

Inawezekana sana, kwa mimi binafsi mtu anaposimama na jazba kubwa, akachana hoja, akasema maneno ambayo mengine hatukuyasikia lakini sijui ya ukali gani, utafikiri Baraza linataka kuripuka humu ndani, mimi nakuwa sielewi. Kwa sababu hiki ni kitu cha usuluhishi. Kama kuna tatizo ndani ya jamii hichi ndicho chombo pamoja na serikali cha kutatua matatizo ya wananchi. Sasa humu kuna agizo ambalo ni *very simple* Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tuliunge mkono ili serikali ifanye taratibu zake kulifanyia kazi. Hakuna jambo jipya au ambalo limeelezwa humu ambalo lipo kinyume na utaratibu na Katiba na Sheria zetu. Yote yaliombwa humu kutekelezwa yapo kwa mujibu wa Katiba yapo kwa mujibu wa sheria zetu. Mimi niwanasihi sana wenzangu, mimi napenda sana umoja wa Wazanzibari na naipenda sana Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, mimi nilianza mapema sana katika kutafuta umoja huu. Mimi nilibahatika kuteuliwa kuwa katika Tume ya Pamoja ya utekelezaji wa muwafaka wa Wazanzibari wa vyama viwili ambavyo ndio mahasimu waliokuwa wakati huo. Mimi naomba sana ndugu zangu wote yaliyopita nyuma tusiyarejeshe leo sio mazuri.

Napata wasi wasi isije ikawa hawa ambao wanazungumza humu Serikali ya Umoja wa Kitaifa haifai pengine ndio wameanza hizi chokochoko huku nje. Napata wasi wasi sana.

Mhe. Spika, mimi nawaomba ndugu zangu kila mmoja kwa imani yake arudi kwa Mungu, msicheze na Mwenyezi Mungu, hana masihara. Nawaomba sana twendeni kwa usalama, tunaelekea kwenye uchaguzi, mwenye kutaka jimbo, mwenye kutaka nchi, twendeni kwa siasa za kistaarabu.

Mhe. Spika: Dakika tano zimekwisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa dakika chache ulizonipa, nakushukuru sana na narudia tena mimi naunga mkono hoja hii ili serikali tuifanyie kazi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana, nakushukuru Mhe. Spika, kunipa fursa hii adhimu na mimi kuchangia juu ya hoja hii binafsi iliyoletwa na Mhe. Hamad Masoud.

Mhe. Spika, kwanza niunge mkono hoja hii ambayo imeletwa na Mhe. Hamad Masoud na ameileta wakati muwafaka kabisa. Mimi naomba Mhe. Spika, uniruhusu ninukuu baadhi ya aya ya tafsiri ya Shekhe Abdalla Saleh Farsi aliitoa katika toleo la nne la tarehe 6 Februari , 1984, ambaye mpaka kufa kwake akiwa ni Kadhi Mkuu wa

Kenya akitafsiri aya namba 135 ya Suratu Nisai, Ukurasa wa 134 ya chapa hiyo yaani Allah (SW) anatoa tangazo na kuwatangazia waumini kwa kusema hivi:-

> "Enyi mlioami, kuweni wenye kusimamia uwadilifu, mtoapo ushahidi kwa ajili ya Allah ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu au juu ya wazazi wenu na jamaa zenu, akiwa yule anayetolewa ushahidi ni tajiri au masikini basi wewe usitizame hilo. Allah anawastahikia zaidi watu hawa, basi msifuate matamanio mkaacha kufanya uwadilifu na kama mkipotosha ushahidi na mkajitenga na ushahidi huo Allah atakuteseni. Allaah anazo habari zote juu ya yale ambayo mnayatenda"

Mwisho wa tafsiri, Shekhe akisherehesha aya hiyo ya Nam. 135 anasema:-

> "Hapana cha kuleta raha kubwa katika masikilizano duniani kama (insab), kusimamia haki hata kama, hapa inahimizwa kusimamia haki vilivyo kweli kweli japokuwa kusimamia haki hiyo kutawadhuru watu wako au kutakudhuru wewe mwenyewe binafsi isaidie haki itande, itapakae kila upande"Mwisho wa kunukuu.

Baada ya nukuu hii Mhe. Spika, namsihi sana Waziri wangu, hii kesi ya serikali dhidi ya dhulma na hii ni kesi ya Kikatiba na Kisheria kwa hivyo namsihi Waziri Mwenzangu ikiwa yeye ni mserikali na mimi ni mserikali. Wengi wamezungumza hapa na wote wametoa tashuhuda zao, kitu ambacho nimekizungumzia katika aya hii, (ushahidi). Nakuomba sana kaka angu, shemeji yangu, kazi yako ilikuwa ndogo sana, imekuwa rahisi sana, wala usipate tabu nenda na ushahidi huo mchukuwe mkurugenzi wako *go field* nenda chini katizame ushahidi huo ni sahihi au si sahihi. (*Makofi*)

Huna kazi wewe tena, kazi yao imekuwa rahisi umerahisishiwa. Wala hakuna mjadala. Wewe nenda *field* sema huu ushahidi nipeni twendeni huko *field* nikachunguze je, huu ushahidi ni kweli hawa watu wamedhulumiwa au laa. Jaribu kutengeneza Husunil-khatima. Kila ukikaa mwenyewe unasali yarabi husunil-khatima.

Husunil-Khatima ndio hii, tengeneza CV yako, tanua CV yako ili leo na kesho iwe wewe ni *reference* kwamba umesimamia haki za binaadamu ndani ya visiwa hivi. Hii ndiyo Husunil-khatima, isimamie, fanya uwadilifu, hao waliokuwa wanakutuma wote ni tantarira tu, siku ya siku ikifika wao wanakuruka, watakuruka hao watakwambia laa hasha mimi nilisema tu. Wewe ndiye mas-ul utaulizwa wewe, haulizwi huyu wala mwengine, wewe si ndiye Waziri, *go field* usikae Ofisini, nenda.

Mhe. Spika, namsifu sana Dkt. Mwinyi alipoletewa taarifa hizi kakaa akasema twendeni na kenda *Alhamdulillah*, kajisafisha niya, ametengeneza ile husunul-khatima na wewe fanya hivyo. Nenda *field* kahakikishe je, hili linalozungumzwa ni kweli, hii si dhana tu. Shemeji yangu *go field,* acha ofisi nenda chini. Simamia uwadilifu huu.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, maneno yako elekeza hapa yatamfika unayemkusudia.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Asante nakushukuru, tengeneza husunul-khatima fil-duniya wafil-akhera, Duniani hapa na huko akhera tunakokwenda.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa sina makubwa nilikuwa namuasa shemeji yangu. Kwa hivyo naomba kuunga mkono mia fil mia. Shemeji yangu kalishughulikie suala hilo, hili ni tatizo, hii ni kesi wewe ni mserikali na mimi ni mserikali hili ni lazima tulihakikishe kwamba wananchi wote wanapata haki zao sawa, nakushukuru Mhe. Spika, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Haya tuweke nidhamu Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Saleh na Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, tusikilize yanayoendelea huko hakuna mkutano. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora na baadaye afate Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

(Hapa vurugu ndani ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi ziliaanza baadhi ya Wajumbe wa Chama cha Wananchi (CUF) na Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi (CCM) walitofautiana na wengine walikuwa wanapiga mabenchi na wengine kupiga mayowe)

Mhe. Spika: Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Saleh, Mhe.Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Mhe. Saleh, Mhe. Hamza Hasan Juma, Waheshimiwa, Waheshimiwa, Mhe. Subeit

Khamis Faki, hebu tusaidie. Mhe. Hassan , Waheshimiwa, Mhe. Hamza, Waheshimiwa, Waheshimiwa Wajumbe. Naomba Kuahirisha Kikao hiki, Waheshimiwa Wajumbe hadi hapo baadaye.

(Saa 4:43 Baraza liliahirishwa kabla ya wakati wake kutokana na kutokufahamiana kwa Waheshimiwa Wajumbe)

(Saa 06.10 mchana Baraza lilirudia)

Hoja ya kuitaka Serikali kuchukua hatua za kuwatimizia Wazanzibari wote waliotimiza sifa za kisheria haki ya kuwapatia vitambusho vya Mzanzibari Mkaazi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru wajumbe wote kwa kuwa wastahmilivu jambo ambalo ni muhimu sana si tu katika shughuli zetu hizi, lakini katika shughuli nyengine zote. Ikiwa mvumilivu basi maisha utakwenda vizuri.

Waheshimiwa Wajumbe, yametokea yaliyotokea hayakuwa yamependeza wala hayakutoa muongozo mzuri kwa wananchi wetu. Sasa kama yaliyotokea hayakutoa muongozo mzuri kwa wananchi wetu basi inafaa tujihusishe kuachana nayo ili tuwe ni viongozi tunaotoa muongozo ulio mwema kwa wananchi wetu.

Baada ya matukio yaliyotokea humu ndani, waheshimiwa humu ndani tulikutana kwa dharura kwa baadhi ya wajumbe wa pande zote mbili wakiwemo baadhi ya mawaziri na wanadhim wetu na tukakubaliana kwamba pande mbili za wajumbe zikutane peke yao halafu waniletee taarifa wa yale ambayo wamekubaliana.

Kwa hivyo taarifa ya kwanza ya Waheshimiwa Wajumbe pande zote mbili waliokubaliana ni kwamba kikao hiki kiendelee katika kipindi cha mchana huu mpaka tumalize kwa kumuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje kutoa hutuba ya kufunga mkutano wetu. Leo kipindi hiki ili tutapotoka humu ndani iwe tumeshamaliza na iwe tumemaliza vizuri kwa kuelewena na kufahamiana.

Jengine ambalo tumekubaliana kwa taarifa niliyopewa, waheshimiwa mawaziri wawili walikwishapata nafasi, upande wa mawaziri kwa upande wa CCM wamekubali kupunguza idadi yao. Kulikuwa na mawaziri wanne ambao bado walikuwa hawajachangia na tayari nilimtaja Mhe. Dr. Mwinyi kwa hivyo wameshauriana na wakakubaliana kwamba Mhe. Dr. tumuombe radhi yeye hatochangia. Lakini vile vile nimearifiwa na upande huo kwamba Mhe. Ramadhan naye alikuwa yumo katika orodha achangie wamekuabaliana na wameniarifu kwamba na yeye hatochangia.

Kwa hivyo kwa upande wa mawaziri wa upande wa CCM waliokubalika wachangie ni wawili. Mhe. Mohammed Aboud pamoja na waheshimiwa Haji Omar Kheri; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ambaye ndie muhusika wa jambo hili.

Kwa upande wa mawaziri wa upande wa CUF ukiachia wale ambao walikwishapata nafasi akiwemo Mhe. Fatma Abdulhabibi pamoja na Mhe. Abdillahi. Vile vile wapate nafasi Mhe. Abubakar Khamis Bakary Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mhe. Juma Duni Haji Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Sasa hayo pia ni makubaliano. Lakini makubaliano mengine ni kwamba tuachane kwa kiasi kikubwa na maneno makali ambayo *unparliamentarily language,* maneno ambayo kimabunge hayakubaliki tuachane nayo.

Maneno ambayo hayaweki heshima kwa mjumbe mwengine tuachane nayo. Maneno ambayo hatimaye yanaweza yakaitwa kwamba ni matusi tuachane nayo, hayo pia yameelezwa kwamba pande zote mbili tumekubaliana twende kwa nidhamu nzuri kwa maneno yaliyo mazuri yale yanayokubalika kwa mujibu wa taratibu zetu za kanuni zetu, bila ya kumtuhumu au kumtukana mtu mwengine.

Mimi napata faraja sana kwamba pande zote mbili hizi zimezingatia kwa makini sana jambo hili na kwa kweli kwangu mimi Waheshimiwa Wajumbe napata faraja kwamba imenisaidia sana, namna ya kuendesha kikao chetu hiki kiende vizuri na kimsingi leo tumekusudia kwamba tumalize shughuli zetu. Kwa hivyo tuondoke hapa tukiwa wamoja, tuondoke hapa tukikubaliana na kuelewana kwamba sisi ni wamoja tena ni ndugu. Lakini tunakubaliana kwamba sisi suala hili la Serikali ya Umoja wa Kitaifa limekuja baada ya kuwepo mivutano mikubwa ambayo

ilidumu kwa muda mkubwa na tukafikia pahala tukaona kwamba hebu tujaribu kwenda na njia hii inaweza ikatusaidia kupunguza *tension* zetu, na ikapeleka maendeleo mbele kwa faida ya wananchi wetu.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru sana kwa ustahmilivu wenu, lakini kuwashukuru sana kwa mawazo yenu mazuri ambayo hatimaye mmeniletea na mkaniambia kwamba haya niyatoe kwenu, ili sasa kila mmoja ajue na afahamu kile ambacho mwenzake au wenzao walizungumza, kumbe tumezungumza tukiwa na mtazamo wa aina moja.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe baada ya maneno hayo ninawashukuru sana kwa uvumilivu wenu, tuendelee kuvumiliana mambo haya ya kisiasa njia yake moja kubwa ni kuvumiliana, bila kuvumiliana hatuwezi tukaenda mbele. Hiyo ndio itatuvusha katika kipindi hiki cha kikao chetu hiki, lakini kwa muda wote mbele tunakokwenda, ili tuendelee kubakia wamoja, tubakie na mshikamano wetu ili tuweze kuendeleza nchi yetu na kuwaongoza wananchi wetu kwa salama na amani.

Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa tuendelee na mjadala wetu kwa namna vile vile tulivyokubaliana. Na kwa maana hiyo sasa nimkaribishe Mhe. Juma Duni Haji Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ili achangie baada yeye tumkaribishe Mhe. Mohammed Aboud Mohammed ili na yeye achangie hatimaye tunamaliza na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na tutamalizia na Waziri muhusika wa jambo hili Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Baada ya hayo basi namuomba sasa Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, achangie kwa dakika kumi zile zile ambazo tumekubaliana mapema.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ninakushukuru kwamba na mimi nimebaki kutoa maoni yangu juu ya suala hili lakini ninashukuru kwamba muongozo wako na wasia ulioutoa unaturejesha katika hali ya kawaida ya kujadili masuala yaliyoko mbele yetu.
Mhe. Spika, mimi sitochukua muda na nadhani nina ushauri na kuweka tahadhari tu ya mambo haya.

Mimi sikufurahia pamoja na kwamba ni mtu wa Chama cha Upinzani suala hili kuchukuliwa kiitikadi. Bila kujali nani aliyeleta hoja ilikuwa ni hoja iliyowasilishwa kuleta tatizo na wenzetu wa *backbenchers*. *Backbenchers* huwa wanajadili mambo ya wizara zetu kulingana na wizara gani iliyoekewa hoja ile na mara nyingi huwa wanaeleza mambo hayo kwa kuwasilisha ushahidi. Na mara nyingi huwa ushahidi wa maandishi na hata taratibu za kibunge na kibaraza la Wawakilishi, unaambiwa hayo unayosema una ushahidi wa maandishi.

Sasa hapa katika kujadili hoja zimewasilishwa nyaraka nyingi sana kuonesha kwamba kuna tatizo kama ni ushahidi wa yale yaliyokuwepo huko yanakofanyika. Kwa hivyo suala la msingi ni kwamba tuna tatizo na hata likafika *stage* likaletwa mbele ya Baraza hili tukufu maana yake tatizo lipo.

Hatuwezi tukakejeli kwamba ushahidi huo ni feki au sio, ni sawa unaweza kuwa ni feki au sio lakini ni ushahidi ulioletwa mbele ya Baraza kusaidia hoja. Kwa hivyo ushauri wangu ulikuwa ni kwamba Mhe. Waziri anayehusika ni kuzichukua nyaraka hizo ambazo nyengine zilishafika hatua ya kungojea kupewa kitambulisho, hatusemi yule kwa sheha au hatusemi yule kwamba hajapewa ruhusa Wilayani lakini watu wameshafika taratibu zote mpaka anapata vile vidude anaambiwa ngojea na bado hapewi, hilo ni suala la msingi.

Mawazo haya yanakuja pengine wala hatumwi lakini wale maofisa walioko kwenye zile Ofisi za Wilaya ama kwa utashi wao au kwa kutumwa na wengine *I don't know* mimi siwezi kuwasingizia. Mimi ninaloweza kulijua nikutolee mfano ni lile la kwetu upande wa Gamba pale, kuna kijana anaitwa Ali Faki, wanakwenda vijana anawaambia hivi hivi tena kwa kiburi kwamba nendeni kokote mnakokwenda vitambulisho hatuwapi. Sasa hii si lugha sahihi wala si shughuli sahihi ya kuwaambia watu huwapi vitambulisho kokote watakokwenda, ilivyotakiwa yeye alinde sheria kama wale waliokwenda kutaka vipande walivyolinda sheria.

Mhe. Spika, *point* ya pili ambayo vile vile sikuifurahia kwamba mjadala huu ukaanza tena kuanza kutajana wapemba, waunguja, wamakonde, wanyamwezi, yeyote ambaye ana haki ya kupata kitambulisho yeye na kabila yake, yeye na anakotoka lakini kwa mujibu wa sheria apate kitambulisho.

Mimi sipendi kutajiwa mambo ya kabila na Mhe. Spika, kwa taarifa yako mara zote ninapokuwa na matatizo na Polisi wakiniuliza kabila yako nani huhamaki ninawaambia mimi sina kabila. Mimi kwetu Kibeni na baba yangu kanambia wewe kabila huna. Sasa ukitajiwa mambo haya ya wapi umetoka, wewe kabila gani haisaidii katika kujenga umoja na si jambo zuri kwa hapa tulipofika. Na wanaonyimwa vipande si wale waliohamia, wanaonyimwa vipande ni wakibeni, ni wadonge, ni wamakunduchi, ni wachaani, ni wakidombo, ni watumbatu, ni wa matemwe. Haiji hoja hapa kama kahamia kutoka Pemba au katika kisiwa chengine.

Sisi tunachosema kila mwenye haki na kufuata sheria na katika huu waraka aliowasilisha Mhe. Hamad Masoud amesema wale wenye haki na waliotimiza masharti.

Mhe. Spika, tatizo la kukosa kitambulisho ninavyoliona mimi hatari yake tunazalisha kundi la watu waliokuwa hawana kwao na kitambulisho zamani ilikuwa ni Serikali inayokwenda huko kwenye vijiji kuwaambia watu wajiandikishe. Ilipokuwa hoja kwamba kitambulisho ndio benki, kitambulisho ndio elimu, kitambulisho ndio tiketi ya kusafiria, kitambulisho ndio kila kitu ndio maana ikawa lazima kila mtu akawa anakitaka. Kwa sababu akikikosa hana maisha, sasa unapomnyima maana yake unamzuia kwamba ashindwe kufanya mengine yoyote yanayostahiki ya haki zake.

Kwa hivyo ninachoogopa ni hicho kwamba tunazalisha makundi mawili, kuna makundi wenye haki wananyimwa na kuna kundi waso haki wanapata; haya yanakua yakikua miaka 10, 20 ijayo ni hatari. Maana hasira inakusanyika kwenye moyo kwa nini fulani kapewa mimi nina haki sikupewa, tunahatarisha maisha ya baadae ya wazanzibari yawe ya hatari.

Mimi sidhani humu kuna mtu aliyekuwa ana chini ya miaka 30, basi ninakupeni nyote miaka 40 muwepo. Lakini miaka 40 ijayo sote humu hatumo. Sasa tusiwaachie kile kizazi kinachokuja matatizo ikawa sababu ni sisi kwa sababu tu ya utashi wa kisiasa.

Mhe. Spika, ninachotaka kukisema Mhe. Hamad Masoud ameweka hoja mezani, ameweka hoja inayosema tuna tatizo, tatizo la kwamba wengine wanapata vitambulisho wengine hawapati. Ushauri wangu Mhe. Waziri anayehusika na suala hili ayachukue haya ushahidi na maoni yaliyotolewa kwamba ni vitu vya kuvifanyia kazi, akae na watu wake huko akatizame wale waliokuwa wametoa vyeti feki asiwape, lakini wale ambao wana ushahidi kwamba wao wanastahiki wapewe jamani. Hatuwezi tukawa miaka yote tunapiga kelele vitambulisho, haiwezekani kwamba sote sisi humu tuwe tunasema uongo, haiwezekani ninahisi Mhe. Waziri achukue ushahidi ulioko mbele hapa aende akaufanyie kazi.

Mhe. Spika, matatizo haya ya wengine kupewa, wengine kukosa nina uzoefu wa nchi mbili katika masuala ya baadae. Suala moja kuna kisiwa kinaitwa Fiji, Fiji wamepata tatizo la aina hii ikafika *stage* mpaka wale wenyeji wazaliwa pale wakahamaki siku moja wakenda kwenye Baraza kama hili wakafanya yaliyokuwa hayapendezi, huo ni mfano mmoja ambao una historia ya ukweli kisiwa cha Fiji, *South Africa.*

Mfano wa pili wa jambo la aina hii ni Saharawi Afrika ya Magharibi kule, watu wa Morocco wamehamia muda mrefu ile nchi ya Saharawi ikafika *stage* wenyeji sasa wanadai haki ikawa ni ugomvi, sasa wale waliozaliwa pale na wale waliokuwa wamekuja, tatizo likawa sasa ni kubwa zaidi ikabidi mpaka Umoja wa Mataifa kushiriki katika kutatua tatizo hilo. Mwenyezi Mungu asitupeleke huko, ninachosema mimi tuna tatizo, tatizo linalohitaji ufumbuzi vitambulisho ni muhimu kwa maisha ya kila siku ya mzanzibari. Anayestahiki kupewa apewe, asiyestahiki kupewa asipewe. Lakini haiwezekani wote ikawa hawastahiki hicho ndio anachokisema Mhe. Hamad Masoud na nyaraka ile aliyoiwasilisha.

Mimi ninashauri pamoja na kwamba maelezo yashatolewa na Bi Mtumwa hapa, mimi sidhani kwamba sivizuri inawezekana kwamba mawazo yangu huyapendi na niliyoyaandika huyupendi lakini daraja ya kufika kuchana waraka katika Baraza la Wawakilishi nadhani si nzuri na haya ndio yanaweza kuwa yakaleta mawazo mabaya.

Mhe. Spika, baada ya mawazo hayo natoa shukurani zangu kwamba tumefika hapa Mwenyezi Mungu ajaalie tumalize salama lakini wanaostahiki kupewa vitambulisho wapewe, wasiostahiki wasipewe. Lakini tatizo lipo na kubwa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza naomba nikuombe uniruhusu kabla ya kutoa mchango wangu nitoe hoja ya muda kwa sababu Mhe. Spika, nikiangalia saa naona ni saa sita na nusu si muda mrefu itakaribia saa 7.00 kwa muda wetu huu wa asubuhi. Inavyoonekana hapa kutokana na hali hiyo ya muda basi kwa vyovyote vile itahitaji tupate muda wa ziada.

Kwa hivyo Mhe. Spika, niliombe Baraza lako tukufu tuweke Kanuni yetu ya muda kando ili tuweze kumaliza shughuli zetu tulizoziweka za kukamilisha siku ya leo hapa baada ya ule muda ambao sio uliomo kwenye kanuni ili tuweze kumaliza shughuli tuendelee. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja Baraza lako liweke muda kando ili tupate muda wa kumalisha shughuli leo, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ni kweli kabisa na hili lilikuwa ndani ya makubaliano nimesahau kulisema, kwamba shughuli zetu tumalize kipindi hiki tulichonacho cha mchana huu na kwa maana hiyo pande zote mbili wameniletea taarifa kwamba wamekubaliana huko, kwamba hoja hii ikitoka basi tuwe tunakubali kuongeza muda mpaka pale ambapo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakuja kumaliza kutoa hotuba ya kufunga mkutano huu. Waheshimiwa Wajumbe, basi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Mhe. Mohammed Aboud sasa endelea zile dakika zako 10 za mchango.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena kuwepo hapa na pia kutupa hekima na busara kwa yale yaliyotokea na tukaweza kurudi tena ndani kwa utulivu mkubwa. Na mimi niungane nawe na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na wajumbe sote kwa kustahamiliana na kuvumiliana ili kuendeleza gurudumu letu la kuwatumikia wananchi.

Mheshimiwa hakuna jambo kubwa kama amani na umoja katika nchi yetu, na sisi tuliomo humu ndani Mhe. Spika kama ulivyosema ndio mfano unaosimamia amani hiyo na umoja huo. Hitilafu ya aina yoyote inayojitokeza kwa upande wetu basi ndio hitilafu ambayo itatokea kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, haitusaidii hata kidogo kutafautiana kitendo ambacho tumekionesha Waheshimiwa Wajumbe cha kuvumialiana na kurudi tena humu ndani, naomba na wananchi wetu wote wawe nacho cha kuvumiliana na kusubiriana ili tuelekee katika uchaguzi mkuu na kufanya mambo yetu katika nchi yetu kwa salama na amani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi nilitulia kwa makini sana kusikiliza hoja na kutafakari kwa kina sana, na nikaona tunao mtihani huko mbele maana kwa njia moja ama nyengine hoja hii imetuleta tumetuhumiana, tumechokozana, tumelumbana na kufikia kutofautiana kwa hali ya vita. Lakini si hilo tu hoja hii kwa kiasi kikubwa imewafitinisha baadhi ya wananchi na serikali yao.

Mhe. Spika, nia na dhamira ya serikali siku zote itaendelea kutenda haki na kuhakikisha kila mwenye haki yake anapata. Suala la vitambulisho ni dhamira ya serikali kufanya kila litakalowezekana, kila mwenye haki, kila aliyetimiza masharti basi kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa taratibu zilizowekwa aweze kukipata. Kwa hivyo, si vyema hata kidogo kufikia mahala tukatuhumiana, tukatafautiana wakati tunazungumzia dhamira moja.

Mhe. Spika, kwa kuwa jambo hili sana ni la kisheria na tunapoliweka kwenye misingi ya kisiasa ndio tatizo linapotokea. Kwa hiyo, mimi niwaombe sana wenzangu bado jambo hili tuliweke katika misingi ya kisheria na lituongoze kisheria ili kuepuka mivutano ya wenyewe kwa wenyewe. Kwa sababu wapo wanaoamini kwamba sheria hii iko sahihi na iko sawa na wapo wanaoamini kwamba ina kasoro. Sasa mahala pekee pakurekebisha hiyo sio humu ndani tena, pahala pekee ni kufuata misingi tuliyoiwekea kisheria kutatua tatizo hili.

Mhe. Spika, naomba ninukuu kidogo ili tuone namna gani tunaweza kupata ufumbuzi yanapojitokeza ambayo yanaweza kutuondoa katika mstari. Mhe. Spika, Sheria hii ya Mzanzibari Mkaazi chanzo chake ni Katiba yetu, ukisoma Katiba kifungu cha 6 (1) kinasema:

“Kutakuwa na Mzanzibari ambaye upatikanaji wake, upoteaji wake na urudishwaji wake atakuwa kama alivyoanishwa katika sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi”.

Kwa msingi huo sheria hii moja kwa moja inakutana na muongozo wa Katiba hii, na katika Katiba hii hii Mhe. Spika kifungu cha 25a (1) kinasema na naomba nikinukuu.

“Mtu yeyote anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu iwapo ataona kuwa Katiba hii imevunjwa au inavunjwa au inaelekea kuvunjwa. Mahakama Kuu itakuwa na uwezo wa:-

a) Kumtaka Afisa yeyote au chombo chochote cha serikali kutoa taarifa inayohitajika na Mahakama Kuu yaweza kufanya hivyo kwa kuombwa au kwa uamuzi wake yenyewe;
b) Kutamka na kutoa amri kuwa Katiba hii imevunjwa au inaelekea kuvunjwa, na Mahakama Kuu inaweza kutoa maagizo ya Afisa anayehusika au chombo cha serikali inachohusika”.

Mhe. Spika, wewe ukitizama kumewekwa mtiririko mzuri wa masharti ya kikatiba ambapo panapotokea tatizo la msingi wa kisheria basi utaratibu wake ni kufuata mkondo wa kisheria ili kuepuka malumbano yake. Na kwa sababu Zanzibar Mheshimiwa siasa iko juu ya ngozi yetu ukiigusa tu hivi, kwa hivyo kwa njia moja au nyengine kwa vyovyote vile tutakavyofanya, kwa mazingira ya hoja hii huna namna ya kuiepuka siasa. Kwa hivyo, msingi wake mzuri ni kufuata masharti ya kikatiba na kuyapatia ufumbuzi kwa utaratibu wa kikatiba kwa mujibu wa sheria zetu.

Mhe. Spika, haiwi sahihi na hata mimi ndipo ninaposema na mimi siwezi kuunga mkono hoja hii, kwa sababu matokeo yake tumeyaona humu ndani na yanaweza kuwa makubwa zaidi nje. Kwa hiyo, utaratibu mzuri ni ule wa kukubali masharti ya kikatiba na sheria hii ikatuepusha kulumbana, kutafautiana na kufikia mengi ambayo yanaweza kutokea katika nchi yetu, kwa sababu njia sahihi na safi ni misingi ya kisheria na ambayo inafaa tuifate na tuiheshimu. Na mara…

Mhe. Spika: Una dakika tatu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Na mara nyingi Mheshimiwa tumesema hapa tuheshimu ule utaratibu wa kila muhimili *separation of power,* na chombo pekee kilichopewa mamlaka kikatiba kutoa tafsiri za kisheria ni Mahakama pale ambapo yanayotokea kuwa tunafika pahala. Kwa hiyo, mimi naomba sana, namuomba sana Mheshimiwa ndugu yangu Mhe. Hamad Masoud hoja yake hii ingekuwa vyema akaipeleka Mahakamani ingepata msingi wa tafsiri wa kisheria na ikatafsiriwa kisheria. Lakini hapa ndani sisi wengine tunaamini kwamba sheria hii iko sahihi, na hasa ukitilia maanani Mhe. Spika kwamba tayari vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vimetolewa, vimetolewa kama ndugu yangu Mhe. Mahamoud alivyoeleza vipo vingi.

Kwa hivyo, kwa njia moja au nyengine yanapojitokeza malalamiko na manung’uniko inakuwa ipo shaka shaka katika utekelezaji wake. Kwa sababu idadi iko kubwa zaidi kwa taarifa nilizonazo mimi juu juu kwamba kuna vitambulisho zaidi ya laki tano na nusu tayari vimeshatolewa. Na ukitizama idadi yetu sasa hivi kwa wale walioandikishwa kama wapiga kura ambao wamefikia masharti ya umri ya miaka 18, utakuta tuko watu kama laki nne na nusu. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile ina maana kuna ziada ya zaidi ya vitambulisho laki moja, kuliko ile idadi halisi.

Mhe. Spika, sasa haya ndio mambo yanaleta shaka, na ndio yanaleta tuhuma kila upande kila mmoja hoja yake anaiona sahihi kutokana na matukio ambayo yanayojitokeza. Kwa hiyo, ndio mimi nashawishika zaidi Mhe. Spika kwa kusema kwamba suala hili ni vyema liende kwenye misingi ya sheria. Na tuondoe sana sana Mhe. Spika masuala ya mazungumzo ya kusema tunabaguana…

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda wako umebakia dakika moja tu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Tumetoka mbali masuala haya ya kuzungumzia ubaguzi hayatusaidii, tumeyazungumza kwa muda mrefu tulifika mahala hatuzikani, tunachukiana, tunalumbana leo *Alhamdulilah* tumefika mahala pazuri.

Si vizuri hata kidogo kutonesha vidonda, kurudishana tulikotoka lazima tunapozungumza kama viongozi tuzungumzie na *spirit* ya umoja mambo ya kutaja taja ubaguzi haya hayasaidii hata kidogo katika nchi yetu. Kwa hiyo, niwaombe sana viongozi wenzangu tunapozungumza mambo ya msingi tuache kulumbana, tuache masuala ya ubaguzi, tuache kuitumia mbinu ya dini katika Baraza. Sote ni Waislamu, sote ni waumini wa Kiislamu lakini Baraza hili si sehemu ya ibada, Baraza hili ni chombo cha kutunga sheria tunakuja hapa kutengeneza hoja.

Kwa hiyo, tusisukumiane halbadiri, tusisukumiane visomo kila mmoja anavijua na Mwenyezi Mungu anaujua ukweli wetu sote; mwenye nia mbaya atahukumiwa na Mwenyezi Mungu kwa nia mbaya yake, na mwenye ukweli basi Mwenyezi Mungu atampa malipo ya ukweli wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nilikuwa nina mambo mengi ya kusema lakini kwa sababu ya muda wako naomba niuheshimu ninachoomba tushirikiane tujenge nchi yetu, tuache tabia za kulumbana, tuache tabia za kugombana tuje na mambo yenye hoja yatakayojenga nchi, tunaelekea kugumu ikiwa leo asubuhi tunaanza kutafautiana, keshokutwa kuna kura ya maoni, mtondogoo tuna uchaguzi mkuu, hebu tuingieni kwa mara ya kwanza katika mambo haya magumu tukifanya uchaguzi katika hali ya amani na utulivu. Hoja ni kushindana kwa sera, kueleza mambo mazuri kwa watu wetu sio kulumbana, kutukanana, kugombana haitusaidii sisi sote ni ndugu. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na halafu nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi.

Mhe. Spika, nafikiri suala tujiulize ni kitu gani tatizo? Mimi nafikiri kuna matatizo matatu, kuna Wazanzibari waliokuwa hawajaandikishwa ambao hawaandikishi, kuna Wazanzibari ambao wameshaandikishwa lakini hawapewi kadi zao na kuna watu ambao sio Wazanzibari na wao wanapewa, hayo ndio mambo matatu yana matatizo. Na tunaposema Mhe Spika kwamba tufuate sheria, tufuate Katiba, tufate nini mimi nakubaliana sana, na nakubaliana na sheria hii iliyopo ingelikuwa tunaifuata hii tusingelipata matatizo kwa sababu ile inasema Mzanzibari aliyefika miaka 18, Mzanzibari anayekaa pale pale kwa miezi isiyopungua sita ndio matakwa yake.

Mtu wa Mgogoni katika jimbo langu amekaa pale miaka yote hata Mkoani hakujui, mtu wa Tumbatu kakaa pale mimi nilikwenda Tumbatu nilialikwa kule nikawaambia wale walionialika basi huyu nitamchukua Mjini, akasema ni bora kwa sababu sijenda kweli akasema Kitumbatu chake miaka yote hajenda Mjini hapa Unguja. Halafu yule unamkosesha kitambulisho kwa nini na utaratibu wote anao.

Mhe. Spika, lakini la pili ilizungumzwa sana hapa suala la rufaa, ni kweli utaratibu wa rufaa ufuatwe, lakini rufaa ina utaratibu wake hutoki tu hujapewa vitambulisho ukenda, ukenda kwa Mkurugenzi au ukenda Mahakamani haiwezekani. Unakwenda katika Ofisi ya Vitambulisho unataka kupewa kitambulisho hupewi unatoa sababu zako kwamba wewe hufai kwa sababu wewe si Mzanzibari.

Wewe hufai kwa sababu wewe hujafika umri wa miaka 18, hapo unakwenda kwa Mkurugenzi, hapo unakwenda kwa Waziri, hapo unakwenda Mahakamani huwezi tu kutoka hapo ukenda Mahakamani, Mahakamani watatupa kesi yako watakwambia kwa nini hukufuata utaratibu. Sasa tusichukue tu kwamba kuna Katiba inasema twende Mahakamani, kuna utaratibu wake.

Kwa hiyo, hiii sehemu hii ya kati kati Mkurugenzi kutoka Ofisi ya Vitambulisho, Mkurugenzi na Waziri ndio penye matatizo. Kwa hivyo, hayo ndio tunayosema yatizamwe.

Mhe. Spika, nakupa mifano miwili ambayo mimi imenitokea mimi mwenyewe bahati nzuri Mhe. Said Ali Mbarouk hayupo, Mhe. Mohammed Aboud alikuwepo lakini kwa bahati katika msafara huo alikuwa na dharura tulitumwa na Mhe. Rais kwenda Pemba katika suala la uandikishaji wa sensa kwenda kuwahamasisha, atakumbuka. Tukenda mpaka Kojani, Kojani tulikwenda mimi *DC* wa zamani ambaye hivi sasa ni *RC* wa Mkoa wa Kaskazini, *RPC* wa Polisi, Mhe. Said Ali Mbarouk tukakaa tukauliza kwa nini jamani hamtaki kujiandikisha? Akatoka mtu akasema mnamuona sheha yule pale, yule tunakaa nyumba zetu hivi uso kwa uso, yaani mlango kwa mlango mimi nakwenda kumwambia nataka kitambulisho ananiambia hanijui, waulizeni Mkuu wa Mkoa anasema hanijui nyumba hizi zimepeana uso.

Sasa leo anakuja ananiambia nikaandikishe sensa niende nikafanye nini na yeye hanijui, ikawa zogo kubwa wakanyanyuka watu zaidi ya 50, utaratibu huo huo sheha anasema hamjui. Mhe. Spika, tukenda tukasuluhisha

tukamwambia Mkuu wa Mkoa hivi sasa alikuwa ni *DC* haya yatatueni, yakatatuliwa huko. Sasa ikifika *stage* kama hizi ndio matatizo yanapokuja Mhe. Spika.

Mhe. Spika, juzi mimi nilikuwepo Pemba, nilikuwepo Pemba nikapigiwa simu kwamba kuna Naibu Sheha wa Msuka amepeleka watu waliokuwa sio kwenda kuandikishwa. Mimi nikampigia Mkuu wa Wilaya pale pale akaangalia akaniambia kuna watu watatu hivi sasa lakini mimi nitawaondoa, sijui kama wale wengine *list* niliyonayo ni watu 17 hapa. Kuna watu watatu nitawaondoa, nikamwambia waondoe. Baadae wakapelekwa watu 13 hawana chochote si wakaazi wa pale, hawajafika umri, hawajafanya chochote lakini walikwenda na sheha wakapewa hivi vitambulisho, majina ninayo hapa Augustine William, John Simon, Bisambe Khatib na wengine wengi hapa. Sasa watu kama hawa ukiwapa wakati wananyimwa Wazanzibari waliozaliwa pale ni tatizo, ndio tunasema hili ni tatizo tusifanye hivyo Wazanzibari wana haki zaidi hawa wamekuja pale hawajatimiza umri.

Kwa sababu hiyo, sheria ya kuwa Mzanzibari lazima ukae pale miaka 15 halafu ukaandikishe, Makamu wa Pili sasa aidhinishe kwamba huyu unamkubali awepo hapa, ndio sheria. Mtu gani katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iliyetolewa barua kusema kwamba huyu namuidhinisha aliyetoka Burundi, Tanganyika, kwamba sasa ni Wazanzibari? Hakuna. Sasa hilo ni tatizo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tatizo jengine kuna watu walipewa vitambulisho sio Wazanzibari bahati nzuri wakenda wakaowa Mkoa wa Kusini Unguja, akamuowa mwanamke Mzanzibari lakini yule mwanamke akamwambia basi twende nikawaone wazee wako (wakwe zangu), kila siku anamshika mpaka akenda akashitaki polisi, aliposhitaki ikawa balaa akaitwa yule kumbe si Mzanzibari kapewa kitambulisho cha Mzanzibari, akenda akahadaa ndugu zetu akaowa kakimbia mpaka leo tukaletewa kesi sisi kwa makadhi, namna gani tutafanya ili aachishwe yule mwanamke. Hayo ndio matatizo kwa nini tunawapa watu ambao si Wazanzibari? Ndilo tunalosema, sasa hili ni tatizo kubwa.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba mtu anahama kwao, anahama Pemba anakuja huku, anahama huku anakwenda Pemba lazima upatikane uthibitisho kama hana uthibitisho sisi hatusemi apewe. Lakini kama kahama kule kaja hapa kakaa kwa utaratibu huo wapewe, lakini hawapewi ni tatizo.

Mhe. Spika, sasa kuna watu wanaokuja wengi wa Tanzania Bara, wa Burundi wapo, wa Kenya wapo hasa ukienda kwenye mahoteli wote wana vitambulisho vya Mzanzibari hawa watatuletea matatizo baada ya muda. Ndio kama ile kesi aliyosema Mhe. Juma Duni ya Fiji ni matatizo. Sasa Mhe. Hamad Masoud Hamad katika hoja yake anasema wale ambao wanastahiki kupewa lakini hawajapewa wapewe, hata kama ni Mzanzibari kama hustahiki sisi hatusemi kwamba upewe ndio tunavyosema.

Mhe. Spika, lakini nasikitika sana hapa nina *message* nimeletewa naomba kwa idhini yako niisome. "Hamna akili ma-*CUF* nyote, wapi mmeona Jeshi likatoa silaha kuwapa maadui wao?" yaani wapi tumeona jeshi hili likatoa silaha kuwapa maadui, maana yake inakusudia vitambulisho ndio ngao ya CCM.

Sasa ikifika *stage* hii na huyu CCM aliyeniletea sijui kama mimi sina akili au yeye, maana yake yeye ndiye anayetafuta choko choko kama hizi tusifikeni huko tunachosema hawa ambao wanastahiki Wazanzibari wapewe vitambulisho vyao, Mzanzibari yeyote aliyekuwa hajatimiza masharti ya sheria asipewe, ndio hoja hii inavyosema. Sasa tukisema kwamba hoja hii haina maana tunasema hapa Baraza la Wawakilishi sote kwamba wale Wazanzibari wanaostahiki tusiwape mimi siko tayari kufanya hivyo, siko tayari kabisa wala Serikali ya Umoja wa Kitaifa haijasema kwamba itawanyima watu haki zao. Serikali ya Umoja wa Kitaifa inasema tutatetea haki za watu, na haki za watu ni pamoja na hili.

Mhe. Spika, mimi naomba sana tusiitizame hoja hii kama ni hoja ya kisiasa au ni hoja ya Mhe. Hamad Masoud au ni hoja ya upande wa upinzani, tutizame hoja hii kwamba ni hoja ya kuwasaidia Wazanzibari ambao wajibu wao wanatakiwa wafanye hivyo. Leo Mzanzibari hawezi kusafiri, leo hawezi kwenda benki, leo Mzanzibari hawezi kufanya chochote kama hana kitambulisho wala hakuna hoja ya kusema aa, kwa sababu nyinyi mlikuwa mkipita mkisema wasijiandikishe. Sasa kama watu wameshafahamu wafanye nini na ndio utaratibu, hufahamu unafahamishwa ukishafahamu unaandikishwa, sasa Wazanzibari wote hawa mtu asiende benki asiende popote.

Mhe. Spika, kwa hayo machache kwa sababu muda ni mfupi na nimesema haraka haraka mimi nakubaliana na hoja hii kwamba wale Wazanzibari waliokuwa wana sifa basi wapewe vitambulisho vyao, wale Wazanzibari waliokuwa hawana sifa na mimi nakubali wasipewe ndio hoja inavyosema. Wazanzibari wale ambao hawajaandikishwa na

wanaandikishwa wende wakaandikishwe na wale waliokuwa si Wazanzibari kama hawa niliowataja na wengine wengi wasipewe mwisho watatuletea balaa katika nchi hii.

Kuna huyu Augustine William hana chochote baada ya miaka 20 atakuja kuomba urais, tushampa kadi hapa tutampigia kura ya urais itakuwa urais ushakwenda huko, pengine ni mtu wa Burundi huyu itakuwa urais ushakwenda Burundi kwa akili zetu hizi tunazozifanya tusifanyeni hayo.

Mhe. Spika, nakushukuru mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja hii kwamba Wazanzibari waliokuwa wanastahiki wapewe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ukimya wa sekundi mbili nilikuwa nikimuomba Mwenyezi Mungu aniepushe na jazba, anijaalie niendelee kumshauri Mhe. Rais kwa hekima na busara katika kazi aliyonikabidhi ya kumsaidia katika wizara hii ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Daima nitaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu anisaidie kwa hilo kwa sababu najua cheo ni dhamana leo ninacho kesho atapewa mwenzangu. Nilikuwemo humu kwa miaka 15 sikujaaliwa kupata nafasi hii, katika kipindi cha miaka mitano inayoendelea sasa nimejaaliwa kwa jaala ya Mwenyezi Mungu kupata nafasi hii. Kwa hiyo, sina uhodari wapo mahodari zaidi wangeweza kufanya kazi hii lakini Mwenyezi Mungu kamtia *ilham* Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kunipa nafasi hii. Namshukuru sana Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuniamini kunipa kazi hii.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ambayo kwa hakika nadhani kwa uzito wa hoja hii unaweza ukanipa upendeleo badala ya dakika 10 ukaniongeza kwa wewe mwenyewe utakavyoona inafaa.

Mhe. Spika, kwa sababu nimeshamuomba Mwenyezi Mungu nisichangie kwa jazba karatasi hizi zote ambazo niliziandika maelezo ya mtu mmoja mmoja naomba niziweke kando na kwa sababu ya lile ulilotuambia sasa hivi tujikite kwenye hoja na wale waliokuwa wametoka nje ya hoja wakawa wanasema maneno ambayo, pengine si mazuri tumepitikiwa. Kwa upande wangu naomba hayo mimi nisiyaguse kabisa na naomba karatasi hizi ambazo zina *gape* karibu 10 nizikunje wala nisizisome, nisome yale ambayo yamezungumzwa kwenye hoja na sheria namna inavyosema. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika, hoja imekuja na imeletwa na Mhe. Hamad Masoud Hamad, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Ole. Mimi nimeitengenezea majibu baada ya kuipata jana na Mheshimiwa kuiwasilisha. Kwa hiyo, maelezo yangu yatajikita katika maeneo mawili, maeneo ya jumla kwa mujibu wa mtazamo wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walivyochangia na kujibu ile hoja yenyewe, yaani kuitolea ufafanuzi kwa mujibu wa sheria. Huko ndiko nitakakojikita Mheshimiwa.

Kwanza nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba wizara hii nimekabidhiwa mwaka jana yaani mwaka 2013 mwezi wa Agosti, nimepokezana kijiti na kaka yangu, mwalimu wangu, Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Mhe. Rais akampa kazi nyengine, majukumu mengine yaliyokuwa kwangu akamkabidhi yeye na majukumu aliyokuwanayo yeye nikakabidhiwa mimi. Kwa hiyo, alinikabidhi pamoja na kazi ambazo alikuwa amezifanya. Sasa nataka niwahakikishie Waheshimiwa wamemtaja sana hapa Mhe. Dkt. Mwinyi na wengine wakamsifu kwamba yeye alikuwa msikivu. Nakubaliana naye kwamba ni msikivu na aliyafanya aliyoyafanya na alinikabidhi pia kile alichokifanya, kile kilichotamkwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba alifunga safari kwenda sehemu mbali mbali kwa ajili ya kulishughulikia tatizo hili na hii ndio misingi ya utekelezaji wa sera sahihi za CCM katika kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, sasa alinikabidhi orodha hii ya Waheshimiwa ambao alifatana nao kupita katika wilaya hadi wilaya na matukio yalikuwa nini kwa hiyo nafahamu. Mimi nilipoingia ofisini niliifanya kazi hii kwa kutaka kujiridhisha ni kwa kiasi gani mambo haya yametekelezwa. Kwa hiyo si kwamba yeye alifanya nilipokuja mimi nikaanza ya kwangu hapana, nilipita nyayo zile zile ambazo amezifanya mwenzangu aliyenikabidhi wizara hii. Kwa sababu maelezo ni mengi kwa ufupi huu ni muhtasari wa ziara wa aliyekuwa Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kadhia hii ya vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na matukio yake na hatua zilivyochukuliwa.

Mhe. Spika, yameelezwa mengi kwamba amekwenda na ikatolewa mfano, kwa mfano ilitolewa *case study* moja hapa ya Wilaya ya Kaskazini 'A'. Kweli alikubali na hiyo kesi ilitolewa na Mjumbe mwenzetu hapa ambaye kwa leo hayupo ndugu yangu Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Chake Chake kwamba kuna watu zaidi ya 3,000 Wilaya ya Kaskazini 'A' wanadai haki hii lakini hawapati fursa hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora alitoka akenda mpaka kwenye ofisi ya wilaya lakini matokeo yake hayakuwa hivyo ambavyo ilielezwa hapa. Sijui walijitokeza watu watatu katika watu 3,000 au hawakujitokeza watu. Sasa hii *experience* ndio inayojitokeza katika suala hili na ndio maana sheria iliweka utaratibu wa kwamba vipi hili suala lichukuliwe hatua, tuli-*handle* vipi serikali ili kuhakikisha watu wenye haki za msingi za kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi wanavipata na serikali imekuwa ikilifanya hilo.

Mhe. Spika, zimetolewa stakabadhi, vimetolewa vyeti na mimi siamini na wala siwezi kuwa na mashaka kwa vitambulisho hivyo ambavyo vimeoneshwa kama vitafika kwenye ofisi zetu za usajili kwa kufuata taratibu halafu visishughulikiwe. Kwa mfano, ndugu yangu jana Mhe. Hija Hassan Hija alionesha zile risiti na jana alinambia angenikabidhi. Bahati mbaya pengine ama amesahau lakini hajanikabidhi, angenikabidhi zile toka jana tungeshakuzi-*verify,* maana yake ukiichukua ile namba tu ya ile risiti ukiiweka pale kwenye *data base* yetu, kwenye *system* yetu inasema kwamba huyu ni kweli kitambulisho chake kimetengenezwa siku falani na sasa hivi kiko wapi.

Nataka niwaambie Waheshimiwa vitambulisho vyote ambavyo vilitolewa risiti vitambulisho hivyo tayari viko *site* ni watu wenyewe wende wakavichukue, maana ndio utaratibu tuliojiwekea. Sasa zile risiti nitamuomba Mhe. Hija Hassan Hija watu wangu wale pale, Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kuna Kaimu Mkurugenzi, kuna mwanasheria na wasaidizi wengine wapo pale wakiondoka zile risiti wawape. Lakini inawezekana usipate kitambulisho pale kwa sababu pengine kitakuwa kimeshapelekwa kwenye *site* ndio utaratibu.

Kwa hiyo, hilo naomba lijulikane wazi kwamba hilo lipo. Kwa hiyo mwenye haki hawezi kunyimwa haki na serikali hii. Serikali ya CCM haina tabia ya kuweza kuwanyima watu haki, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina utaratibu wa kuwanyima watu haki.

Mhe. Spika, lakini katika maelezo ya jumla limejitokeza pia suala la vyeti feki.

Mhe. Spika: Dakika zako Mhe. Waziri zimebakia tatu kati ya dakika kumi, umeomba nyongeza nakuongeza na tano una dakika nane.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, niongeze 10.

Mhe. Spika: Loh, naona ni mnada hebu tuone hizo tano kwanza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Haya. Mhe. Spika, vyeti *fake* vipo, vyeti *fake* hii ni *sample* Kitumbatu tunaita sampuli. Hizi ni sampuli za vyeti *fake* na vyeti hivi sio kwamba wamejiamulia wao tu watu wa Idara ya Usajili wa Vitambulisho wanawasiliana na wenzao wa Urajis wa Vizazi na Vifo kuthibitisha haya. Kwa hiyo, vyeti *fake* vipo na msingi wa ku-*verify* vyeti ni kwamba tunajua kuwa watu wapo watafanya udanganyifu ndio maana tuna-*verify* vyeti. Kwa hiyo, mawasiliano yapo kati ya Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo na Idara ya Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, tukigundua humu kuna vyeti *fake* hivi ni vyeti *fake* na vyeti vyengine hivi unamkuta mtu ana vyeti viwili ana kitambulisho ameshatengeneza, lakini ana kitambulisho anataka kutengeneza kwa cheti chengine. Hayo yote tumeyagundua Mhe. Spika, muda ni mdogo.
Vyeti ambavyo vimegundua feki *sample* ya Unguja tu 146, kwa hiyo, kwa nini Serikali tusi-*verify* kuhusu suala la kuangalia vyeti. Kwa sababu hata unapotafuta *passport,* kithibitisho cha kwanza ni cheti cha kuzaliwa. Kwa hiyo, na sisi tumekiweka cheti za kuzaliwa kama ni kithibitisho cha ku-*verify* masuala ya vyeti. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa tusipuuze hilo.

Lakini suala la kadi za utambulisho, Wilaya zote za Unguja vitambulisho ambavyo vimekaa karibu ya miaka mitatu, mbali ya vile ambavyo alivionesha Mhe. Dr. Mwinyi Haji wakati ule na sheria yetu inasema vikishakaa miaka mitatu tuviangamize, maana hivyo vitakuwa havina wenyewe na havina wenyewe kweli, kwa Unguja ni vyeti 66,870 na kwa Pemba ni vyeti elfu 7182.

Hebu vionesheni hapo watendaji si mnavyo na hivi tunasuburi kibali cha Idara ya Mazingira tu kwa sababu vimesha-*qualify* kwamba havistahiki kuwepo kwa muda miaka mitatu wenyewe wanatafutwa hawapo na kwa nini hawa wenyewe ni vipi. Hawa wenyewe ni watu wakuja kwa matukio, yaani wanakuja wakati ya matukio likimaliza lile tukio wanaondoka, wengine wako Uingereza, wengine wako Tanzania na wengine wako wapi. Wanakuja kwa matukio.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Hebu haya masanduku, hebu yalete hapa mezani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Wanakuja kwa matukio Mhe. Spika, na Wazanzibari wakaazi hawaji kwa matukio. Wazanzibari wakaazi wanakaa katika maeneo yao kisheria na kihalali.

Mhe. Spika, Limezungumza suala la sheha. Sheha ana *register,* yaani ana buku lake la wananchi wanaoishi kwenye eneo lile. Sasa unapompuuza sheha hutaki kujisajili, kilelezo chake ni *register*. Waheshimiwa naomba tuwasihi wananchi wetu wafate taratibu waji-*register* kwa sheha kama ni wakaazi wa eneo lile ili sheha aweze kuwa hana sababu ya kumkataa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Vitambulisho vilivyosalia katika vituo. Utaratibu uliopo wa rufaa. Utaratibu wa rufaa ni kwamba sheria inasema; "Mtu anapokosa kupewa hali yake kama Mzanzibari Mkaazi anatakiwa ende kwa Mkurugenzi" na zipo kesi ambazo zimeshughulikiwa kupitia kwa Mkurugenzi. Bahati nzuri hizo zilizofika kwa Mkurugenzi zimetatuliwa wala hazikuja kwa waziri na anapokosa haki kwa Mkurugenzi, aje kwa waziri.

Mimi karibu miaka miwili nimeshakuwa waziri pale sijapata mtu yeyote kuja kwangu kama amenyimwa kwa Mkurugenzi, kwa hiyo, anakata rufaa kwa waziri na anapokuwa kwa waziri hakutendewa haki, utaratibu wa kikatiba wa kwenda Mahakamani upo na zipo kesi tatu zimeshaamuliwa Mahakamani. Kwa hiyo, rufaa inafanyakazi; ipo kesi iliyomuhusi Mwadini Mzee Abdallah, ipo kesi iliyomuhusu Mussa Abdallah Hemed na ipo kesi iliyomuhusu Mohammed Saleh Saidi, nazitaja kwa sababu hizi zimeshatolewa maamuzi.

Kwa hiyo, si kweli kabisa kwamba mtu anaponyimwa haki kwa Mkurugenzi, akinyimwa haki kwa waziri hawezi kwenda Mahakamani akapata haki, akienda Mahakamani atapata haki yake, akija kwa Mkurugenzi atapata haki yake kama anastahiki na akija kwa waziri kama anastahiki kwa nini nimnyime.

Mhe. Spika, Tumeambiwa tuangalie *Husna-al- khatima,* kila mmoja anajali hilo na ndio maana Mwenyezi Mungu mimi naijali sana hiyo *Husna-al- khatima* na ndio maana nafanya yale amabayo ametuamrisha Mwenyezi Mungu mengi, sitaki nijisufu lakini mengi mishatimiza na mengi nayafanya na nikijaali kiinua mgongo cha safari hii nitekwenda tena Hijja kwa mara ya pili. *Ummar* ni kawaida yangu, hiyo ndio *Husna-al- khatima.* Sadaka najitahidi na Zakkat najitahidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilitaka niseme hilo kwa sababu kesi zipo ambazo zimetolewa. Orodha ya Shehia ya idadi na rufaa zilizoshughukiliwa tokea mwezi wa Disemba 2010. 2010 rufaa zilizishughulikiwa ni 405. Kwa hiyio, wanaokata rufaa wanapata haki zao. 2011 rufaa zilizoshughulikiwa na wakapata haki zao ni 28, 2012 ni rufaa 59 kwa wale wanaonyimwa huko kwengine wakifika kwenye ngazi wanatapa hizo haki zao. 2013 ni rufaa 236 rufaa zimeshughulikiwa na 2014 ni rufaa 61 zilizoshughulikiwa.

Lakini jengine nataka niseme *sample* ya *copy* ya cheti hiki baada ya ku-*verify* tumegundua kwamba cheti hiki ni cha mtu mwengine kwa mujibu wa namba za usajili wa Idara ya vizazi na vifo. Kwa hiyo, lazima Serikali tuwe makini katika hii haki ambayo inapigiwa kelele sana na Serikali hii inafanya haya kwa kutaka kutimiza hizo haki za watu wanaostahiki kupata haki zao wapewe haki zao.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, nataka niseme vile vile kwamba ni kweli tumeshafanya chaguzi hapa na chaguzi hizo ili uingie kwenye *register* la kura au la mpiga kura sharti uwe na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Ninazo

takwimu hapa za matokeo yan uchaguzi kuanzia mwaka 2010 mpaka hivi sasa, iwapo kama ingekuwa wanabaguliwa wa CUF na CCM kama Wajumbe walivyosema si dhani kwamba takwimu zingekuwa zina-*turn* kama zinavyokuwa.

Uchaguzi wa mwisho wa mwaka 2010 ulikuwa asilimia 50.1 kwa CCM na 49.1 kwa CUF, kama ingekuwa sisi tunatoka kwa CCM tu hata mgepata hata asilimia 10, isingekuwa hivyo. Lakini 2005, ni 53.2 kwa CCM na 46.1 kwa CUF. Sasa haya ndio matokeo ya uchaguzi sasa hatutoi vitambulisho kwa sababu ya siasa kwanza nataka niseme hilo.

Kwa sababu ya muda Mhe. Spika, ninayo hoja ambayo nilikuwa najibu hoja za hoja iliopo mbele. Lakini kwa sababu ya muda, naomba hii ichukuliwe iingie kwenye *Hansard,* mimi nimenukuu sheria kwenye *Hansard* na Sera ya vitambulisho, tamko la sera linasema nini, naomba ninukuu Mkakati wa sera kipengele kimoja tu (a) kinasemaje:-

(a)Kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni na Taratibu zinafuatwa katika hatua zote za usajili na utoaji wa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi na kwamba kitambulisho kitatolewa kwa wale tu wanaostahiki. Wanaostahiki ni wale Wazanzibari wakaazi katika eneo husika hawa watapewa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, vitambulisho hivi vimekaa hakuna wenyewe, siku moja kule Pemba Mhe. Suleiman Hemed alisema atawaleta watu fuso tatu kwa watu waliokuwa wananyimwa haki ya vitambulisho. Bahati mbaya baada ya kuleta watu fuso tatu, alipeleka watatu watatu. Sasa haya ni mambo ambayo tunayakuza lakini uhalisia wa mambo haupo, *sample* hiyo moja, lakini ziko nyingi za namna hiyo.

Kwa hiyo, mimi nasisitiza Mhe. Spika, tupo hapa na Serikali ipo kwa kutekeleza sheria ambazo tumezipitisha sisi wenyewe, kama tunahisi sheria ina mapungufu, tufate utaratibu wa kisheria tuje turekebishe sheria hivyo tunavyoona itaondosha mapungufu, lakini kwa sasa tutafata sheria ambayo ipo, hatuwezi sisi kutokufuata sheria iliyopo maana ndiyo tuliyoitunga na ndiyo ambayo watunda sheria wamempelekea Rais na Rais akaisaini na ndio inayotumika.

Sasa tukitaka ibadilike ni lazima sisi watunga sheria tufanye utaratibu wa kisheria turekebishe sheria. Lakini kwa sasa hiyo sheria ndiyo iliyopo na mimi niwasihi wananchi mara nyingi wanapopata makatazo kutoka kwa sisi wanasiasa tunajaribu sana kuyafata lakini athari zake ni kubwa. Mimi sitaki nende huko niwaombe wananchi makatazo mengine tunayokuwa tunapewa tuyaangalie kwa umakini sana, kwa sababu yanaweza yakatuketea athari.

Lakini mimi nasema nitaendelea kufuata sheria, wengine hapa wamesema tutasomeana halalbadiri tusifike huko, maana wengine hizo halalbadiri tuna vitabu zaidi ya 20 vya halalbadiri. Sasa si dhani kama iyo itatusaidia kutujenga sana. Lakini tuzungumze lile la msingi na mimi nasema kwa yale yote ambayo wameyasema Waheshimiwa Wajumbe kwamba wananchi wapewe haki zao ndivyo sheria inavyosema, tufate tu utaratibu, yeyote anaenyimwa Wilayani aje kwa Mkurugenzi, akinyimwa kwa Mkurugenzi aje kwa Waziri na nikimnyima mimi waziri ende Mahakamani, huo ndio utaratibu wa kisheria. (*Makofi*)

Ni kweli Mhe. Jihadi ni shemegi yangu na namshukuru alinileta kitu nikapata kitu mtoto mmoja, namshukuru sana. *First born* wangu nimempata kutoka kwao, kwa hiyo, namshukuru sana kwa hilo hakuna tatizo. Lakini mengine yote yale Mhe. Spika, naomba tufate utaratibu, tufate sheria iliyopo ili tuweze kuwatumikia wananchi Wazanzibari vyema. Tatizo hapa linalogoma kwamba rufsa kwa mujibu wa sheria ni mwananchi mwenyewe anatakiwa ende akalalamike, haya maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa ni haki yao na ndio maana mimi nimeyafanyia kazi nikaweza kupata huu ushahidi na maelezo na vielelezo ambavyo vipo katika idara yetu na watendaji wale nataka niwapongeze sana wanafanyakazi nzuri sana na wala hakuna maagizo ya mkubwa yeyote yule ambayo wanapelekewa kuangazia ngazi ya sheha mpaka ngazi ya Idara ya Usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi.

Mimi kama waziri sijatoa maelekezo hayo na wala sijatoa maagizo hayo, Rais hajafanya hivyo. Sasa tusije hapa tukasema maelekezo, maagizo hakuna kitu kama hicho Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendeshwa kwa mujibu wa Utawala wa Sheria; sheria, sheria. Ahsanteni sana naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe: Spika, Mhe. Waziri tunakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe pia nawashukuru. Sasa kabla sijamwita mtoa hoja, nadhani hiki kitu tushakiona ya kutosha.

Sasa niwaombe watendaji waondoe taratibu bila ya ghasia ili Mhe. Haji Omar Kheri akanidai kwamba imepotelea humu ndani. Sasa watendaji na yale masanduku tuvikusanye kwa utaratibu kabisa wakati namwita Mheshimiwa mtoa hoja sasa aje kutoa majumuisho. Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, *Assalamu alaikum*.

Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu kwa mara ya kwanza maishani mwangu kwa kukubali hoja yangu binafsi niiwasilishe katika Baraza lako tukufu hili.

Mhe. Spika, kitendo hiki kwako wewe kukifanya ni adimu sana, lakini *Alhamdulillah* kwa hili Mwenyezi Mungu amekujaali, nakushukuru sana.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja kwa sababu ya wakati ili niwatambue wale ambao wamechangia hoja hii binafsi iliyowasilishwa na mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Ole.

Mhe. Spika, hoja hii binafsi imechangiwa na Wajumbe wako 38 kwa kusema, mmoja kwa maandishi na mimi nikiwa miongoni mwa hao ambao wanachangia hoja hii, itakuwa imevunja rekodi. Itakuwa imechangiwa na Wajumbe wako 40 kamili.

Wajumbe ambao wamechangia hoja hii ni kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Hassan Hamad Omar
2. Mhe. Ashura Ali Sharif
3. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
4. Mhe. Mohammed Haji Khalid
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
6. Mhe. Saleh Nassor Juma
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
8. Mhe. Hija Hassan Hija
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
10. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
11. Mhe. Salim Abdalla Hamad
12. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
13. Mhe. Marina Joel Thomas
14. Mhe. Asha Abdu Haji
15. Mhe. Mgeni Hassan Juma
16. Mhe. Subeit Khamis Faki
17. Mhe. Mussa Ali Hassan
18. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
19. Mhe. Kazija Khamis Kona
20. Mhe. Farida Amour Mohammed
21. Mhe. Ali Salim Haji
22. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
23. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
24. Mhe. Salma Mohammed Ali
25. Mhe. Rufai Said Rufai
26. Mhe. Hamza Hassan Juma
27. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

28. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
29. Mhe. Haji Mwadin Makame
30. Mhe. Haji Faki Shaali
31. Mhe. Machano Othman Said
32. Mhe. Fatma Abduhabib Ferej
33. Mhe. Abdilah Jihad Hassan
34. Mhe. Juma Duni Haji
35. Mhe. Mohamed Aboud Mohamed
36. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
37. Mhe. Haji Omar Kheir
38. Mhe. Bikame Yussuf Hamad

Mhe. Spika, kwanza kabisa Mwenyezi Mungu kwa jaala yake amenijaalia tangu hoja imechangiwa mpaka sasa hivi sikupata kusinzia, sikupata kutoka nje ya ukumbi na nimejaribu kadiri inavyowezekana kunakili kila ambacho ni muhimu sana kunakiliwa, ili nikija kutoa majumuisho hapa nisiwe na wasi wasi kama hili nimelisikia au sikulisikia, yaani hili nimeliandika au sikuliandika.

Mhe. Spika, lakini Hoja hii Binafsi kwa bahati yoyote kama ni mbaya au nzuri imejaribu kuchafua hali ya hewa kidogo hapa. Hii inaonesha kwamba hii hoja ni nzito.

Mhe. Spika: Tupige makofi kwa nidhamu ili tumalize kazi hii vizuri. Mhe. Hamza, ninakuomba sana.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, nasema hoja hii imetengua kidogo Baraza lako, lakini hii ni ishara na dalili kwamba hii hoja ni nzito, si nyepesi. Kwa sababu ingekuwa ni hoja nyepesi, kwanza isingelichangiwa na idadi kubwa kama hii. Idadi kama hii huchangiwa katika bajeti zile ngumu. Nyinyi muna uzoefu lakini watu 40 kuchangia hoja hii ambao wengine wanasema ni nyepesi. Mimi ninasema ni hoja nzito sana na ushahidi mmoja ni huo.

Kwa hivyo, haya ambayo yametokea umeeleza vizuri. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed ameeleza na mimi nimuombe Mwenyezi Mungu anijaalie niwasilishe hoja hii bila ya kutengua tena Baraza hili. Semeni *Amin*! basi.

Mhe. Spika, niwapongeze wote, nina-*underline* neno "wote" Wajumbe wako watukufu 39 waliochangia hoja hii. Musiwe na wasi wasi aliyeteleza ulimi akasema lugha ambayo humu hairuhusiwi, ikinilenga mimi mtoa hoja, huyo nimemsamehe duniani mpaka akhera. Hata wale waliochana hoja hii mbele ya Baraza hili, nao wamepata msamaha wangu. Ni demokrasi lakini pia inawezekana ni mughma. Ninasema wote hao nimewasamehe. (*Makofi*)

Na hakuna lililoniudhi au kunikera na kama muli-*notice* wakati wote wa pukurushani zile, mimi nilikuwa makini sikuondoka kitini, kwa sababu nilijua nina kazi ngumu sana mbele ya Wajumbe watukufu, Wajumbe makini wa Baraza lako hili.

Mhe. Spika, na mimi nimefurahi sana kwamba wewe mwenyewe upo kwenye kiti ukishuhudia hoja hii inavyojadiliwa na Wajumbe wako watukufu sana sana na ninakushukuru kweli kweli.

Mhe. Spika, kwa kifupi mjadala wote huu wa hoja hii tangu mwanzo mpaka mwisho, niligundua kwamba yalikuwa ni mambo maarufu ambayo ni *very common,* ama kasema Mjumbe huyu au yule, yamerudiwa yakikaririwa ni haya mambo yafuatayo.

Wengine wamepongeza hoja na mtoa hoja, wameunga mkono na wengine wamesikitika sana kwa nini hoja hii nimeileta Barazani na bila ya kisisi au kikakasi kakasi au kigugumizi hawakutafuna maneno, wamesema hawaungi mkono hoja hii.

Jengine ambalo limezungumzwa sana ni ushahidi na vielelezo mbali mbali wa nakala za vyeti vya kuzaliwa, Stakabadhi za kuchukulia *Zan-ID*. Kiitikio kwa Wajumbe wengi waliozungumza ni namna masheha wanavyokataa kutoa fomu. Fomu ambazo kisheria lazima uwe nayo ndiyo uwende ngazi nyengine ama ya Wilaya au ya Mkurugenzi au ya Waziri.

Watu wameeleza hapa umuhimu wa *Zan-ID,* uvunjwaji wa Sheria Na. 7 ya 2015, yaani Serikali namna ambavyo imevunja sheria hii. Ziara ya Waziri aliyekuwa anashughulikia vitambulisho, jirani yangu, kaka yangu, rafiki yangu Dkt. Mwinyihaji Makame aliyoifanya Pemba tarehe 16/07/2013 na 17/07/2013, mimi mwenyewe nikiwa nimeambatana naye.

Hatua kadhaa zilizochukuliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kadhia hii, vile vile, kuna wengine wamemtaka Makamu wa Pili wa Rais kwamba ametoa amri kwa masheha kudai vyeti vya kuzaliwa.

Jengine ambalo limeonekana linaguswa sana ni mtu asiyekuwa Mtanzania kupewa *Zan-ID*. Ushahidi hapa ulielezwa kwamba haya yalitendeka Mhe. Hamza Hassan Juma akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa walipotembelea hoteli moja iliopo Kaskazini Pemba.

Kuwepo kwa vyeti feki vya kuzaliwa, kuwepo kwa *Zan-ID* ambazo hazijachukuliwa hadi sasa. Idadi mbali mbali ya majimbo zenye watu wenye sifa na hawajapewa fomu na sheha hadi sasa. Mkurugenzi kuwakimbia umma wa zaidi ya watu elfu mbili kule Chake Chake ambao aliagiza waletwe ili awaone kama ushahidi. Vifungu kadhaa vya Katiba ya Zanzibar ya 1984, Toleo la 2010 na vya Sheria Na. 5 na Na. 7 ya 2005.

Jengine ni jinsi wanyonge wanavyogharimika na kuhangishwa na Serikali bila ya mafanikio ya kupata *Zan-ID*. Jengine ni wageni kupewa *Zan-ID* bila ya kutimiza sifa na masharti ya kisheria.

Baadhi ya Wajumbe wametaka nieleze ni kwa nini hoja hii imekuja wakati huu. Kwa nini hoja hii imeingizwa hapa kisiasa. *Zan-ID* kufanywa mtaji wa CCM. Maagizo ya aliyekuwa *DC* Kaskazini "A", Bi. Riziki kuzuia watu kupewa fomu lakini akaamrisha mmoja wao apewe kwa simu. Jengine ni watu kunyang'anywa Stakabadhi bila ya kupewa *Zan-ID* katika Wilaya ya Kaskazini "A".

Mhe. Spika, jengine ni masheha kuweka Kanuni zisizokuwepo na zilizo kinyume na Sheria hii ya Na. 7 ya 2005. Baadhi ya Wajumbe wamependekeza kuifanyia marekebisho Sheria hii Na. 7 ya 2005 na wengine walisema kwamba Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein aingilie kati jambo hili.

La mwisho, lakini si kwa umuhimu ni Serikali kuwa chanzo cha tatizo hili la vitambulisho.

Mhe. Spika, nimefanya *summary* ya yote kwa sababu karatasi hii ya *A4* nimeandika *page 39* michango ya Wajumbe. Sasa Mhe. Spika, naomba niendelee kama ifuatavyo.

Chimbuko la Hoja hii na kwa nini inaletwa wakati huu.

Mhe. Spika, hii imekuja wakati huu kwanza Kanuni za kuleta hoja kama hii haikupangwa iletwe lini. Lakini kubwa kuliko yote ni namna suala hili lilivyoshughulikiwa katika daraja mbali mbali kabla ya kufikishwa hapa na walioahidi kulishughulikia wakawa kama mchezo wa kuigiza, wanaahidi lakini hawatekelezi.

Lakini vile vile ni baada ya uvumilivu wa muda mrefu wa kilio hichi na kwamba Serikali haikuonekana kuwa sikivu na ilikuwa inafanya tashititi. Niwakumbushe Wajumbe wa Baraza hili tukufu hatua ambazo zimechukuliwa tena nyengine ndani ya Baraza hili, lakini hakuna chochote kilichoonekana kutekelezwa, ilikuwa ni malumbano, tashititi, kejeli, dharau kwa wale wanaotoa kilimo chao kwa Serikali.

Mhe. Spika, baada ya mjadala katika mkutano wa Baraza la Januari, 2013 aliyekuwa Waziri anayehusika na *Zan-ID* ni Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame aliahidi katika Baraza hili kwamba atafuatana na Wawakilishi kwenda Wilaya hadi Wilaya, ninamshukuru sana. Hili Mhe. Dkt. Mwinyihaji alilitekeleza na alifanya vikao kila Wilaya. Walioshiriki katika vikao hivi ni yeye mwenyewe, Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi wa Wilaya husika na majimbo husika, Mkurugenzi wa Vitambulisho, Wakuu wa Wilaya na Mikoa, Madiwani, watendaji wa Ofisi za Vitambulisho kutoka Unguja na waliopo Pemba, lakini walioshiriki kikamilifu kwa kuhudhuria ni masheha wote ambao wako katika Wilaya fulani.

Mhe. Spika, katika vikao hivi mengi yalibainika. Mhe. Dkt. Mwinyihaji ni shahidi kwa maelezo yaliyokuwa yanatolewa na yeye mwenyewe, Mkurugenzi wa Vitambulisho, Wakuu wa Mikoa na baada ya nafasi kutolewa kwa masheha na wengineo waliokuwepo pale. Sheha wa Mtambile alitamka bila ya kisisi kumwambia Waziri, hayo ni

mambo yenu sisi hatukubali, tutafanya tunavyoona kwamba tufanye. Yupo, Wawakilishi wa Mkoani wapo, Wabunge wa Mkoani hapa hawapo.(*Makofi*)

Ndipo hapa tulipoona kwamba mbona hapa kuna kiini macho, inakuwaje leo Sheha aliyechaguliwa na Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa yupo chini ya Wizara ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji, inakuwaje leo Sheha hana kisisi na hakuna yoyote iliyochukuliwa. Inawezekana Sheha alipongezwa na akaambiwa uzi huo huo. Kwa sababu baada ya kuondoka pale, yeye ndiye aliyekithiri yale aliyokuwa anafanya alizidisha mara mbili.

Hotuba za Waziri, Mkurugenzi na ma-*RC* zilikuwa tamu kama asali. Yaani unajua kabisa hotuba hii leo tatizo hili limeondoka. Baada ya vikao vile vyote vinne kwa Wilaya nne za Pemba, Masheha walikaza buti wakazidisha ile ari, jeuri na kibri. Haijatokea hata siku moja amri ya Waziri ikawa ndogo kuliko ya Sheha na kama hiyo inatokea na inaruhusiwa, basi inaonesha ni namna gani utawala bora usivyofanyakazi katika nchi hii.

Mhe. Spika, leo mimi kuleta hoja hii ni mahali pale, ni wakati wake na sisi tunawajibika kulishughulikia hili. Sisi Waheshimiwa nawakumbusha Sheha ni mtu wa Serikali na Mkurugenzi wa Vitambulisho ni mtu wa Serikali, wajibu wetu sisi ni kuisimamia Serikali, hasa pale ambapo tunaona kwamba kuna ulegevu. Kazi haifanywi kama Serikali inavyotaka ifanywe, ni lazima tuwasimamie na jukumu hili msijivuwe Waheshimiwa Wajumbe, mmeajiriwa na wapiga kura ili kuwafanyia kazi wao.

Mhe. Spika, kama hiyo haitoshi kwa nini hoja hii imekuja. Watu wamesema hapa kwamba waende Mahakamani. Mbona Mahakamani watu wameshakwenda. Masheha saba, ili umshitaki Sheha unaishtaki Serikali, ili uishtaki Serikali unatoa *notice* ya siku 60, wanaonyimwa haki hii kwa maana kwamba wana sifa zote, lakini hata Sheha hawapi fomu. Walijikusanya wakaenda kwa wakili, wakili akatengeneza kesi akapeleka *notice* na *notice* hiyo ilikuwa *failed* tarehe 31 Oktoba, 2014.

Kwa hivyo, mpaka tarehe 30 Disemba, 2014 siku 60 zilikuwa zimekwisha, hadi leo hakuna lolote ambalo waliopeleka *notice* ile wameambiwa. Kwa hivyo, kutoka Januari, Februari na huu Machi karibu siku 90, tangu *notice* ile ilipofika muda wake kwa ku-*mature.*

Mhe. Spika, kama hilo halitoshi, si mnasema hatwende Mahakamani, Masheha wa Shehia tano, baada ya kuona huku Serikali, maana inaonekana hii ni *syndicate*, basi wacha tufanye *mandamus application*. Wanasheria wanaijua, waka-*file case* Mahakama Kuu tawi la Chake Chake. Sasa ni karibu mwezi wanaambiwa hatujapata Hakimu au Jaji wa kesi hii, hiyo ndio hali.

Kwa hivyo, mnavyozungumza muende Mahakamani, kwa Mkurugenzi au wapi. Hebu fanyeni *research,* hivi vyombo vya Mahakama vyote ni vyenu, kwa nini hatutaki kuona tatizo lilipo, kwa nini hatutaki ukweli. Kwa hivyo, Mhe. Mohammed Aboud, hii najibu hoja yako, kwamba ni hayo kwa hayo maji ya futi na nyayo. Huna popote kama mmedhamiria vitambulisho msitowe, huna popote utakapokwenda ukapata kitambulisho. Mahali peke yake ni hapa kuwajibisha mawaziri, ni hapa hapa wala hakuna mahali pengine na msiukimbie ukweli.

Mhe. Spika, kama hilo halitoshi tumetumia Kanuni kabisa ya Baraza hili. Kikao kilichopita, mimi na Wawakilishi wenzangu watano, tulimuomba Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ Mhe. Haji Omar Kheir yule pale, tukutane naye alikuwa kidogo ni mgumu, lakini baadae akasema sawa, baada ya kumuambia kwamba huna haja ya kufanyo woga, hili ni jukumu lako na hii ni Kanuni. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakitaka kumuona waziri wakati wowote, wanaweza kumwita wakalizungumza. Akabisha bisha hii ni *caucus*. Sio *caucus* ni Wawakilishi, *caucus* ya *CUF* ni Wawakilishi wote, ni baadhi ya Wawakilishi.

Tulikutana katika ukumbi huo mdogo hapo juu, tukamueleza kadhia hii mwanzo hadi mwisho. Alituahidi na alitunasihi kwamba ndugu zangu, rafiki zangu na jamaa zangu sisi ni wamoja, suala hili niachieni baada ya wiki mbili nitawatafuteni popote mlipo ili hili tulijadili. Wenzangu wote nimewauliza, je, yuko yeyote aliyepigiwa simu na Mhe. Haji Omar Kheir katika hili, hakuna aliyejitokeza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mambo mengine sisi Waheshimiwa hapa kuna mawaziri na kuna *backbenchers,* kuna mambo mengine hapa kwa sababu ya kawaida ya Baraza hili hatufukuwi makaburi na ndio maana tunamwita waziri kumuomba na kumnasihi, ni wajibu wetu, tungekuja hapa tukapasuka. Hadi leo hii sio wiki mbili, sio tatu, wala sio nne, yule pale kimyaa. Hii sio dharau ni nini, kwa nini utudanganye, tuambie tu kwamba suala hili mimi msiniambie, lakini siku

zote hizo tunasubiri tu hadi leo huyo hapo. Leo Mhe. Waziri ana maneno mengi sana, ni wakati wake. Mtu mzima akivuliwa nguo huchutama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nikiwemo mimi mwenyewe tumefanya vikao mbali mbali. Mimi nilifanya kikao na *DC* wa Wete mara mbili, ili kueleza matatizo yalioko Jimbo la Ole na Masheha wake. Akanipa maelezo marefu, lakini hatimaye tukakubaliana kwamba atawaita Masheha na kwamba Masheha atawaambia wafuate taratibu.

Mimi Mhe. Spika, sijaona sheria ambayo watekelezaji wako wa mwisho wanasheria yao nyengine. Mimi mtu aniambie popote katika Kanuni zake, kwamba ili upewe fomu kwa Sheha lazima iwe wiki nzima kwa siku moja, yaani Masheha wameweka wiki nzima siku hii moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kule Ole ni siku ya Ijumaa. Sisi ni wawakilishi msisahau, sisi tunabebeshwa na tunaelezwa mambo chungu nzima, wametutuma hapa tuwatetee haki zao, kwa hivyo, wanapokuja ni lazima uwasikilize na hatua ionekane imechukuliwa. Ijumaa hiyo hiyo ambayo wameweka tulikwenda, tena nilikwenda na waandishi wa habari na nilimuambia Mkuu wa Wilaya nakwenda Ijumaa na waandishi wa habari kama mmesema ni Ijumaa tu. Tumekwenda katika ofisi ya Sheha wa Mchangamrima saa 10:00, maana yake amesema Ijumaa baada ya sala ya Alaasiri, saa 10:00 tumekaa mpaka saa 11:30 ofisi inalala na kufuli ya Sheha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumekwenda kwa Sheha wa Ole Mussa Ali, tulipokwenda kule ana maneno mengi, mimi mpaka nisali, sawa. Mhe. Spika, baada ya sala kuna wanachama zaidi ya 50 wenye vyeti tena niliwaambia chukuweni *original*. Akasema ilivyokua mmenijia na waandishi wa habari basi mimi fomu hizi, akatoa fomu zaidi ya 200, hizi hapa fomu anatusukumia. Nikamwambia hapana, sisi tumekuja. Kumbe siku moja kabla aliwaambia watu kwamba sina fomu hata moja, yaani ni udanganyifu na ni ubabaishaji tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumekwenda Kiuyu Kiongoni, Sheha wa Kiuyu Kiongoni Juma Haji, ametoa fomu mbili halafu akafunga mlango hakuonekana kwake. Tukawaambia watu mbakie hapa hapa mpaka saa 7:00 za usiku, hakurudi mpaka alfajiri kwake maana yake ni nini. Hii yote ni kuthibitisha kwamba Masheha ndio tatizo na chanzo na nyinyi hamtaki kukata pua mkaunga wajihi na ndio hapa watu wengi wanasema hii ni *syndicate,* sababu zinazotolewa ni za ajabu ajabu. Huyo Sheha ukimkuta anakuambia leo sina fomu, fomu iliyobaki ni moja tu sijatoa *photocopy*, mbona mmekuja watano leo.

Sasa wewe wiki nzima siku moja, tuje wangapi, wengine wanasema tumeambiwa tusitowe, nani kakuambia aah! mwawajua nyinyi huko wakubwa wenzenu, mwengine anakuambia sina muhuri, mwengine anakuambia kamati yangu ya kusaini hizo fomu hawapo leo. Yaani ni ubabaishaji na ushughulishaji watu, ilimradi sijui ni nini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naeleza sababu kwa nini hoja hii imekuja hapa. Mhe. Spika, kuna majibu maalum ya watu maalum. Hoja ni kwamba hapa si mahala pa kufanyia siasa na hoja hii imekuja kisiasa. Hebu mjumbe gani aniambie hapa hatoki kwenye chama cha siasa, nani kaja hapa na charahani kushona sidiria, nani kaja hapa na mshipi kuvua ndio kazi zetu, wote tunatoka katika vyama vya siasa, sisi ni wanasiasa mkitaka msitake na Baraza hili kabla ya Katiba toleo la 2010, mlikuwa na *RC* Wakuu wa Mikoa humu uongo. Wakuu wa Mikoa wakaambiwa nyinyi sio wanasiasa tokeni, leo unaposema kwamba hapa tusifanye siasa, siasa ifanywe wapi, nyote ni wanasiasa nyinyi na hapa ndio pakufanya siasa, ambaye hataki kufanya siasa *out*. Kuna *professions* mbali mbali, hapa Maalim Abuu yule pale ni *lawyer*.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda umetumia mkubwa kidogo, sasa nikuombe umalizie katika muda wa dakika 10 ili twende kwenye hatua nyengine...

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Muda, Mhe. Spika, wajumbe 40 sio mchezo. Sikusikii Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Muda uliokwishatumia ni mkubwa kidogo. Kwa hivyo, nakuongeza na dakika 10 nyengne umalize. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Ushahidi wa mwisho kwamba hapa ni mahali pa siasa, sitaki nikumbushe kilio matangani, lakini siku ya hoja ya kura ya maoni hapa, zogo likaibuka, wengine wanasema CCM na wengine wanasema dalali, ikawa kama ni nyimbo, kama sio siasa ni nini hiyo, nani kaamrisha yale, si wanasiasa wetu.

Mhe. Spika, tunajiuliza hapa wahalifu wa sheria hii ni wengi, kwa mujibu wa sheria hii yeyote ambaye ana sifa za kupata *Zan-ID*, ametimiza sifa na masharti ya kisheria na hana, angalieni kifungu, iko *penalty*. Hebu mimi niambieni ni lini kakamatwa mtu mmoja tu sitaki wawili kwamba hana *Zan-ID* na ametimiza masharti na akapelekwa Mahakamani, hakuna. Makisio yanasema watu waliotimiza sifa na masharti ya kisheria na-*underline* maana yake ndio hoja yangu na ambao wamenyimwa kwa makusudi, kwa kuanzia na Masheha maana yake ndiko chemchem iliko ni zaidi ya 30,000.

Sasa leo mtu akiniambia kwamba waliosajiliwa ni wengi sana kuliko wanaotarajiwa. Mhe Spika, *statistically* kama tuna 1.3 *million people,* watu wenye umri wa miaka 18 ambao wanatakiwa kuwa *voters*, *statistically* ni *58 percent,* hiyo ni kama 740,000. Imetolewa idadi hapa na Mhe. Mahmoud Mohammed, Mhe. Spika, idadi ile ina kasoro kubwa mno, inakisiwa 5 *percent* ya idadi ile ni *under age,* wako chini ya umri.

Mhe. Spika, nilishuhudia siku ya Jumamosi ofisi ya vitambulisho Mkoani, sio siku ya kazi na nilipewa taarifa tu, nenda Mkoani ukaone uchafu unaofanyika. Nilipokwenda kuna watoto wadogo zaidi ya 300 wamewekwa kwenye tawi la CCM, wanachukuliwa kidogo kidogo wanapelekwa kwenye kituo cha kupigia kura, wamechukuliwa watatu, watatu wanapelekwa kule wanapigwa picha, wameletwa pale kwa magari ya abiria kutoka Kiwani na kutoka Mkanyageni, hiyo ni siku ya Jumamosi, tusemeje katika hili.

Mhe. Spika, unamuuliza Mkuu wa Vitambulisho Pemba anagwaya tu, anasema mimi hawakuniambia, wamefanya vibaya leo wasamehe, hayo yametokea. Leo mnasema kwamba hapa utaratibu ufuatwe na hivi na hivi. Wewe kama jicho lako limeoza usimwambie mwenzako kwamba wewe jicho lako lina tongo.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, malizia na usitoke nje ya mipaka tukenda tusikokusudia.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, umuhimu wa *Zan-ID* umeelezwa. *Zan-ID* kwa Mzanzibari ni maisha; hupati ajira, hupati kusafiri nchi za nje kwa sababu hupati *passport,* hupati hata kufungua *account* ya benki, hupati leseni ya kuendesha gari, huwezi kupata fursa ya kumchagua kiongozi unayemtaka. Kwa ufupi bila ya *Zan-ID* maisha Zanzibar ni magumu. Sasa katika hali kama hiyo na Serikali hii ambayo inapenda watu, kwa nini tatizo hili kubwa la kila siku, kilio kisichokwisha msilimalize. Hivi kweli Serikali hii inashindwa kuondoa tatizo hili wakikusudia kweli kweli, hawashindwi, hawataki. Ndio maana sababu nyingi hapa zinatolewa kukinga tu,yaani hoja hii sio ya msingi, hoja hii imeletwa wakati sio, hoja hii imeletwa kisiasa. Hii ni hoja makini.

Mhe. Spika, niseme kwamba mimi hoja hii sikuileta leo hapa Barazani, tarehe 23
niliwasilisha hii mezani kwako wewe, tarehe 23 Januari, hii...

Mhe. Spika: Umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, sijafika hata nusu kuwajibu wajumbe, ndio wajumbe 40 sio mchezo, hii kazi nimeikusudia mimi sikuja hapa kufanya mchezo, kwa kifupi Mheshimiwa kwa dakika hizo hizo zilizobakia, kwa mwelekeo wa Baraza hili na amri ambazo zimetoka kwa Naibu Mnadhim ni kwamba watu wa CCM wote wakatae, namshukuru ndugu yangu Mwakilishi wa Bububu kama atakataa kwa amri sawa, lakini ashakubali kuunga mkono hoja hii.

Muhimu kuliko yote hoja hii ikakubalika au isipokubalika kwanza Mheshimiwa mimi katika hoja hii sibadilishi hata koma, isipokuwa ukurasa wa nne *paragraph* ya tano, katika mkutano wa Mei, 2015 na hii imo kwenye *Hansard* nikasema katika Mkutano wa Mei, 2005 kwa sababu hoja hii ilikuwa ije kabla ya *March*. Kwa hiyo, katika hili hoja hii ndio mahali pake Serikali mumepewa ushauri mbali mbali na wengine mmekiri kwamba tatizo ni lipi na tatizo lipo, hoja hii ni makini kwa sababu isingekuwa makini wewe mwenyewe Spika, usingeruhusu, huruhusu upumbavu hapa, huruhusu upuuzi, suala tu linakuwa na tatizo unamwita mtu unamwambia hebu rekebisha hapa, hebu fanya hivi.

Leo hoja kama hii hoja nzito Mhe. Spika, ameikubali mpaka kuletwa hapa na sio kama kaikubali hivi hivi tu, imepita kwenye *panel* yake, yaani *legal panel*, leo mtu anakwambia hoja hii siju ni vipi, ni vipi ni vipi, mimi narudia tena kwamba tatizo lipo, Serikali mkitaka kuliondoa tatizo hili Makamu wa Pili wa Rais unasikia wewe ndio mtendaji mkuu wa shughuli za Serikali katika Baraza hili na sio Baraza hili tu hata shughuli za Serikali huko nje.

Tafadhali, tafadhali Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama ni siasa iwache, unaongoza watu ambao wana tofauti ya itikadi, wanatoka mwahali mbali mbali, tenda haki uweke rekodi; kama Mwenyezi Mungu kakujaalia uendelee kuwa ndio kakujaalia, kakujalia uwe Rais utakuwa, lakini kama hakukujaalia kwa kufanya haya maisha huwi.

Mhe. Spika, nashukuru sana wakati wako, lakini kama Gen Okello aliyeshiriki kikamilifu Mapinduzi ya Zanzibar alifukuzwa hapa, leo unakuja kumpa Mmakonde asiyekuwa na sifa hata moja *Zan- ID,* inafanana hiyo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa kwa maana hiyo basi sasa niwahoji, wanaokubaliana na hoja hii pamoja na maazimio yake wanyanyue mikono,makatibu angalieni vizuri, wanaokataa. Inaonekana waliokataa wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, mimi na macho yangu mabovu niliona kama waliokataa kidogo ni kidogo, hebu na tuwahesabu *(Makofi)*

Mhe. Spika, natumia hiyo kwa mujibu wa Kanuni nikiwa nina wasi wasi tuhisabu nataka tujue *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: Mheshimiwa Mnadhimu alikuwa tayari anatoka na amerudi kusikia nini kitakachoendelea, mimi kauli yangu nilisema inaonekana waliokataa wameshinda, mkanyamaza kimya, ndio nikasema basi tumemaliza. Sasa kiutaratibu hasa hili suala la kuhisabu kura lipo, kabla ya kumaliza pale Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ulikuwa utoe hiyo hoja ya kwamba kura zihesabiwe ili niwaambie makatibu wahesabu kura.

Mimi nadhani tukubaliane na huu uamuzi, ila nataka niseme jambo moja kukataliwa kwa hoja hii maana yake nini, kwamba ofisi inayohusika iendelee kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria, sio kwamba sasa ifunge virago isifanye kazi aa, kwa sababu hii ili ifanye kazi kwa mujibu wa sheria wengi mmezungumza humu ndani. Kwa hivyo, maelekezo ninayotoa kwamba Ofisi inayohusika ya usajili wa vitambulisho na wengine wote wanaohusika wafanye kazi kwa mujibu wa sheria, tumemaliza hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, nataka kutumia muda mfupi sana kuwashukuru kumaliza kikao hichi ambacho niseme kilikuwa kigumu kidogo, lakini ndio kawaida ya vikao hivi, kwamba tumemaliza salama nichukue nafasi kuwashukuru wajumbe wote kwa mashirikiano hayo, lakini nitoe shukurani maalum kwa watendaji wakiongozwa na Katibu wa Baraza ndugu Yahya Khamis Hamad na watendaji wengine wote kwa kazi nzuri tuliyofanya kufanikisha mkutano huu wa kumi na tisa. Tuwashukuru wenzetu waliotusaidia kurusha matangazo haya na pia waandishi wengine wa habari na baada ya maelekezo mbali mbali watendaji wengine wa Serikali waliitikia na wakawa wamehudhuria katika vikao vyetu jambo ambalo nataka liwe utamaduni wa kudumu.

Unapokuwa na shughuli kama hizi basi watendaji waje ili kusikia maelekezo mbali mbali yanayotoka hapa kupitia Wizara zinazohusika, nichukue nafasi hii kuwashukuru wote na sasa nichukue nafasi kwa heshima kubwa kumkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Karibu.(*Makofi*)

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kumaliza Mkutano huu wa 19 wa Baraza la Wawakilishi kwa salama na amani. Pia, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuliendesha Baraza letu hili tukufu kwa hekima, busara na ustahamilivu mkubwa. Uwezo wako wa kuliongoza Baraza hili ndio uliotuletea mafanikio makubwa katika mkutano huu.

Aidha, napenda kumshukuru Mhe. Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti kwa kukusaidia kuuendesha Mkutano huu wa 19 kwa umakini na ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, kwa aina ya kipekee naomba kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa umahiri, hekima na busara kubwa hali ambayo imeiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na kudumisha amani na utulivu wa nchi yetu. Vile vile, natoa shukurani kwa Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Spika, nachukuwa fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi zao nzuri katika kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa maagizo ya Kamati mbali mbali za Kudumu za Baraza hili, taarifa zinazohusu sekta zao na kutoa majibu kwa hoja mbali mbali zinazotolewa na Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Spika, nawashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa maswali waliyouliza juu ya utendaji wa Serikali na michango, mapendekezo na maelekezo yao waliyotoa wakati wa kujadili Miswada na hoja mbali mbali zilizowasilishwa hapa Barazani. Ni dhahiri kwamba, michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi inasaidia sana katika kuimarisha utendaji wa Serikali.

Mhe. Spika, kabla ya kuelezea mafanikio tulioyapata katika Mkutano huu wa 19 kwa masikitiko makubwa naomba kuchukua nafasi hii kumkumbuka mwenzetu ambaye alikuwa Mjumbe wa Baraza hili Marehemu Salmin Awadh Salmin, aliekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni aliyefariki tarehe 19 Februari, 2015. Marehemu alikuwa ni kiongozi hodari, mwenye msimamo thabit, makini na shupavu na aliejitolea kuwatumikia wananchi kwa kipindi chote cha uhai wake.

Hatuna budi kuyaenzi na kuyaendeleza yale yote mazuri ambayo ametuachia kwa manufaa ya nchi yetu. Kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naendelea kuwapa pole Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza, wanafamilia na wananchi wote kwa ujumla. Sisi sote ni waja wake Mwenyezi Mungu na bila ya shaka marejeo yetu ni kwake. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. *Amin.*

Mhe. Spika, katika Mkutano huu wa 19 jumla ya maswali ya msingi 62 na maswali ya nyongeza 147 yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Aidha, jumla ya Miswada minne (4) imewasilishwa,kujadiliwa na kupitishwa na Baraza lako Tukufu.

Miswada hiyo ni:

a. Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Usajili na Usimamizi wa Wathamini na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

b. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

c. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Namba 6 ya 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki na Sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonyesho Namba 1 ya 2009 na kutunga Sheria mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo MengineYanayohusiana na Hayo.

d. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano Namba 1 ya 1999 na kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, Baraza limejadili na kupitisha Sheria ya Kuweka Masharti ya Usajili na Usimamizi wa Wathamini na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo kwa madhumuni ya kuweka utaratibu wa kisheria wa kusajili na kusimamia wathamini. Pia, sheria hii inapendekeza mfumo mpya wa kuanzisha bodi ya wathamini ambayo itakuwa na utendaji na ufanisi na yenye kukubaliana na mabadiliko ya kitaaluma na fani ya uthamini.

Mhe. Spika, Serikali inawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mapendekezo yao waliyoyatoa ambayo yametoa mchango mkubwa katika kupatikana sheria hii.

Mhe. Spika, mswada wa pili uliowasilishwa Barazani ni Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Kamisheni ya Ardhi na

Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Lengo kuu la mswada huu ni kuanzisha sheria itakayosimamia masuala ya ardhi katika kujenga uimara wa uongozi na usimamizi wa ardhi kwa ajili ya matumizi bora na maendeleo ya Taifa. Aidha, mswada huu unapendekeza kuanzishwa kwa Kamisheni ya Ardhi kwa ajili ya kuongoza na kusimamia masharti ya sheria hii pamoja na sheria nyengine zinazohusiana na masuala ya ardhi.

Mhe. Spika, Serikali inawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa michango na maoni yao yaliyopelekea kupatikana kwa sheria hii ambayo itasaidia sana katika kuweka utaratibu wa matumizi bora ya ardhi na kupunguza migogoro ya ardhi nchini.

Mhe. Spika, mswada mwengine uliowasilishwa ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Namba 6 ya mwaka 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki na Sheria ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho Namba 1 ya mwaka 2009 na kutunga Sheria mpya ya Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Madhumuni ya kufuta sheria hizo na kuanzisha sheria mpya, ni kuimarisha utendaji wa kazi na kusimamia majukumu ya kulinda na kuhifadhi mila, silka na maadili mema ya Wazanzibari na kutumia utamaduni katika kupunguza umasikini kwa jamii.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena Serikali inawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao ambayo ilisisitiza zaidi katika kulinda na kudumisha mila, silka na maadili mema. Ni mategemeo yetu kwamba, tutapata mashirikiano makubwa kutoka kwa wananchi katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, mswada wa mwisho uliowasilishwa katika mkutano huu wa 19 wa Baraza lako Tukufu ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Miradi ya Maridhiano Namba 1 ya 1999 na kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kuanzishwa na kuendesha mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Binafsi na Mambo MengineYanayohusiana na Hayo. Madhumuni makubwa wa Mwaada huu ni kuweka vipaumbele katika kuendeleza miundombinu ya kitaifa kwa mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi katika kukuza uchumi endelevu na mendeleo.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe pia walipata muda mzuri wa kuchangia na kutoa maoni juu ya kuimarisha mswada huo. Ni imani yangu kwamba kupitishwa kwa mswada huu utasaidia kuimarisha uwazi na ushindani usiofungamana na mgongano wa kimaslahi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwa ujumla, Miswada yote hiyo ilikuwa na lengo la kutunga Sheria zenye kuimarisha, kukuza na kuendeleza uchumi wetu, kujenga mazingira mazuri ya utawala bora na uwajibikaji pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji na upatikanaji wa huduma za kijamii. Ni imani yangu kwamba, kupitishwa kwa sheria hizo kutarahisisha utekelezaji na usimamiaji wa mipango ya Serikali kwa watendaji wake na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, pamoja na Miswada hiyo, katika Mkutano huu wa 19 Serikali pia iliwasilisha mbele ya Baraza lako Sheria ya Kura ya Maoni Namba 11 ya 2013 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Kifungu 132 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kwa ajili ya kuridhiwa na Baraza ambapo sheria hiyo ilipata ridhaa ya Baraza.

Mhe. Spika, katika Mkutano huu pia Baraza lilipokea na kujadili Ripoti za Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Kudumu za Baraza kwa mwaka 2013/2014. Taarifa hizo zilichangiwa kwa kina na Waheshimiwa Wajumbe na Waheshimiwa Mawaziri walitoa ufafanuzi wa hoja zote zilizotolewa. Nachukua nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati na Wajumbe wao kwa kazi kubwa walioifanya ya kuihoji, kuishauri na kuielekeza Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Naamini haya yote yalifanyika kwa nia njema kuisaidia Serikali kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba, Serikali imezipokea Taarifa za Kamati za Kudumu za Baraza na itayafanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Mhe. Spika, vile vile katika Mkutano huu wa 19 Baraza lako Tukufu lilipata nafasi ya kupokea Taarifa ya Kamati Teule ya Kuchunguza Upotevu wa Nyaraka. Namshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati Teule Mheshimiwa Mahmoud Mohammed Mussa na Wajumbe wake wote kwa taarifa yao kwa Baraza na nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia hoja hii. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri walioitolea ufafanuzi hoja.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba, Serikali imepokea Taarifa ya Kamati Teule na kupokea michango yote iliyotolewa katika Baraza. Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa na kutokana na michango ya Wajumbe na hatua muafaka zitachukuliwa kwa wale wote waliohusika na kadhia hii. Ni kweli kabisa kuwa tukio hili lilikuwa la kusikitisha sana.

Mhe. Spika, Baraza pia lilipokea na kujadili hoja binafsi ya Mheshimiwa Hamad Masoud Hamad inayohusu Ucheleweshaji wa Upatikanaji wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kuhusu suala hili, kwanza napenda kuwanasihi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuepuka jazba na utashi wa kisiasa wakati tunapojadili hoja mbali mbali hapa Barazani na pia tukumbuke kwamba, masuala mengine ni ya kisheria, sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe. Suala la kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ni suala la kisheria na kila Mzanzibari anastahiki kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa kisheria.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa ujumla wakaelewa kwamba, Serikali hii haitamnyima haki Mzanzibari yeyote aliyetimiza masharti ya kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Ni wajibu wetu Viongozi kuwaelimisha wananchi wetu juu ya utaratibu wa kisheria uliopo na kuwataka kuufuata utaratibu huo bila ya kuweka shindikizo za kisiasa.

TAARIFA ZA KISEKTA

Mhe. Spika, kilimo bado kinaendelea kuwa ni mhimili mkuu wa uchumi wetu na ndicho kinachotoa ajira kwa wananchi walio wengi, kwa kutambua hilo Serikali inaendelea kutekeleza programu na miradi mbali mbali ya kilimo. Juhudi hizi zimepelekea kuimarika utoaji wa elimu kwa wakulima wa mazao ya chakula, biashara, viungo na matunda, matumizi ya pembejeo, matumizi ya zana za kisasa za kilimo ikiwemo matrekta na miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu 2014/2015, matayarisho ya msimu wa kilimo cha mpunga yanaendelea ambapo jumla ya matrekta 32 yamekuwa yakitoa huduma kwa wakulima. Kazi hii imekuwa ikifanyika kwa mafanikio makubwa ambapo hadi sasa jumla ya ekari 16,197 kwa Unguja na Pemba zimeshatayarishwa. Aidha, Serikali imenunua na kusambaza kwa wakulima jumla ya tani 225 za mbolea ya *TSP*, Urea tani 600, dawa za kuulia magugu lita 15,000. Pia, tani 146 za mbegu zimenunuliwa na kusambazwa. Napenda kutoa wito kwa wakulima wote kukamilisha shughuli zao za kilimo ili kuzitumia vizuri mvua zinazoendelea.

Mhe. Spika, katika kuendeleza matumizi bora ya ardhi nchini *(Land Use Planning),* Serikali imekamilisha Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Ardhi wa Zanzibar. Utekelezaji wa Mpango huu utasaidia kupunguza matumizi holela ya ardhi. Sambamba na Mpango huo, Serikali imetayarisha Sheria ya kuanzisha Kamisheni ya Ardhi itakayosimamia matumizi yote ya ardhi nchini. Aidha, Serikali imeendelea kuziimarisha Mahakama za Ardhi kwa kuzipatia vitendea kazi na kuziongezea idadi ya Mahakimu. Juhudi zote hizi zimelenga katika kupunguza tatizo la migogoro ya ardhi lililodumu kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inaendelea na jitihada zake za kuwapatia wananchi wake huduma bora ya maji safi na salama. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imeendelea kutekeleza Miradi na Programu mbali mbali za kuwapatia wananchi wake maji safi na salama pamoja na kuendeleza Mpango wa Kulinda Vyanzo vya Maji Unguja na Pemba.

Vile vile, Serikali imeifanyia matengenezo makubwa miundombinu ya usambazaji maji katika maeneo mbali mbali mjini na vijijini ili kuhakikisha kuwa huduma ya maji inapatikana kwa wananchi wakati wote bila ya usumbufu. Aidha, Serikali imechukua hatua maalumu ya kuziondosha mita 41 za TUKUZA zilizokuwepo katika visima mbali mbali vya miradi ya maji ili kuwaondoshea kero wananchi na kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama bila ya usumbufu. Lakini hapo hapo ningependa kuwanasihi wananchi kwamba waache kuvichafua vianzio vya maji kwa kujenga katika vianzio hivyo.

Mhe. Spika, Sekta ya Utalii imeendelea kuimarika. Idadi ya watalii walioingia nchini imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia watalii 274,619 mwaka 2014. Ongezeko hili linatokana na kuimarika kwa miundombinu ya utalii pamoja na hali ya amani na utulivu uliopo nchini. Nawaomba viongozi na wananchi wote kuendelea kudumisha amani katika nchi yetu hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu ili utalii wetu uzidi kuimarika na uchumi wetu uzidi kukua. Nawasihi sana wananchi wawe wakarimu kwa wageni wetu

wanapokuja kututembelea ili isadifu ile kauli mbiu yetu ya "*UNGUJA NI NJEMA ATAKAE AJE*". Ukarimu wa Wazanzibari unajulikana duniani kote.

Mambo Mengineyo:

Mhe. Spika, katika kipindi kifupi kijacho wananchi wote wa Tanzania watapata nafasi ya kuipigia Kura ya Maoni Katiba Inayopendekezwa, Katiba ambayo kama itakubalika ndio itakayoliongoza Taifa letu katika kipindi cha miaka 50 ijayo. Kufanyika kwa kura hiyo kutakamilisha awamu ya tatu ya mchakato wa uandikaji wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanafanya maamuzi sahihi siku ya tarehe 30 Aprili, 2015, nawasihi wananchi kuisoma kwa makini na kuielewa Katiba hiyo inayaopendekezwa na maamuzi yao yatokane na matakwa na ridhaa zao binafsi na siyo kushawishiwa na watu, vikundi au vyama vya siasa.

Katika kufanikisha hilo Serikali imegawa nakala za Katiba inayopendekezwa kwa wananchi Tanzania nzima ili waisome, waielewe na kuifahamu. Ni imani yangu kuwa Watanzania wote wataitumia fursa hii adhimu na adimu kuhakikisha nchi yetu inapata Katiba kwa kwenda kupiga kura ya maoni kwa amani, utulivu na usalama.

Mhe. Spika, vile vile mwaka huu wa 2015 ni mwaka wa Uchaguzi Mkuu hapa nchini. Wananchi watafanya maamuzi ya kuwachagua viongozi watakaowaongoza akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Ni imani yangu kwamba, wananchi watajitokeza kwa wingi katika kuitumia nafasi hiyo ili kuwachagua viongozi wao pamoja na kujitokeza kugombea nafasi za uongozi kwa wale wenye sifa za kufanya hivyo.

Aidha, Serikali kwa upande wake inaendelea na maandalizi ya uchaguzi huo ikiwemo uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura, kutoa elimu ya uraia na upatikanaji wa vifaa vya upigaji kura. Sambamba na hayo Serikali itahakikisha kwamba chaguzi zote hizo zinafanyika katika hali ya usalama na amani kwa kutovifumbia macho vitendo vyote vinavyoashiria uvunjifu wa amani.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii nitoe wito maalum kwa viongozi wote wa kisiasa na wa kijamii pamoja na wananchi kwa ujumla tushirikiane na Serikali katika kuendeleza na kudumisha amani na utulivu uliopo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa hivi karibuni nchi yetu ya Tanzania imeingia katika wimbi la utekaji na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino). Mengi yamesemwa kuhusu sababu za matokeo haya. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalaani kwa nguvu zote suala hili na iko pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua inazoendelea kuchukuwa katika kukabiliana na tatizo hili. Kwa mnasaba huu nachukua nafasi hii kutoa wito maalumu kwa wananchi kuongeza mapenzi na huruma baina yetu katika kuwalinda na kuwathamini wenzetu hawa.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kuwa hivi sasa tuko katika kipindi cha Msimu wa Mvua za Masika. Mwanzoni mwa Machi, 2015 Mamlaka ya Hali ya Hewa ya Tanzania kanda ya Zanzibar ilitoa taarifa ya muelekeo wa mvua za masika kwa kipindi cha Machi hadi Mei 2015. Mvua hizo tayari zimeshaanza na zinaendelea. Ili kujikinga na majanga na maafa yanayoweza kutokea katika kipindi hichi yakiwemo maradhi ya mripuko na mafuriko, nachukua nafasi hii kuwakumbusha wananchi kudumisha hali ya usafi wa mazingira yetu yanayotuzunguka na kushirikiana na Baraza la Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote za Unguja na Pemba katika kuchukua hatua madhubuti za kuweka maeneo yetu katika hali ya usafi ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza.

Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Afya itaendelea kuielimisha jamii juu ya madhara yanayoweza kutokea pamoja na hatua madhubuti za kujikinga na maradhi mbali mbali yanayoweza kutokea katika kipindi hiki.

Mhe. Spika, vile vile, naomba kuchukua nafasi hii kuwakumbusha wananchi hasa wakulima kukitumia vizuri kipindi hiki cha mvua za masika tunachoendelea nacho katika harakati za kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Aidha, Serikali itaendelea kushirikiana na wananchi katika upandaji wa miti ya kudumu ili kuweza kuongeza uhakika wa upatikanaji wa chakula na matunda na kuinua hali ya kiuchumi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda kuwatanabahisha Waheshimiwa Wawakilishi wote kwamba mambo yaliyotokea ndani ya Baraza letu Tukufu tarehe 11 Machi, 2015 wakati wa kuwasilisha mbele ya Baraza Sheria ya Kura ya Maoni Na: 11

ya mwaka 2013 ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa kifungu 131(2) cha Katiba ya Zanzibar mwaka 1984 yamewasikitisha wananchi wetu wengi. Na hata yaliyotokea leo wakati wa kujadili hoja binafsi ya Mhe. Hamad Masoud Hamad, kuhudu upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari, yaliyotokea mnayajua, sina haja ya kuyaeleza kwa kirefu lakini mambo hayo hayakuwakilisha vizuri Baraza letu mbele ya macho ya wananchi wetu tunaowawakilisha. Wananchi wetu wengi wametuona kama tumekuja kucheza badala ya kufanya kazi waliyotutuma. Kuhitilafiana kwenye Baraza ni jambo la kawaida lakini ni vyema busara ikatumika badala ya jazba.

Nasaha zangu kwenu tunaposhughulikia mambo ya Kitaifa tuweke kando jazba zetu. Nawaombeni siku zote tufanye kazi tukielewa kuwa wananchi wetu wanatufuatilia matendo yetu ndani ya Baraza na watatuhukumu. Naomba sana wakati tukiendesha shughuli zetu ndani ya Baraza hili tuweke mbele umoja, upendo na mshikamano ili wananchi wetu waendelee kutuamini.

Mhe. Spika, mwisho kabisa, kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru tena kwa dhati kabisa wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kuliendesha Baraza letu kwa umakini mkubwa. Vile vile, nawashukuru Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu kwa kutekeleza majukumu yao vyema kwa mashirikiano makubwa na kukusaidia vyema katika kutekeleza shughuli za Baraza. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa ushiriki wao katika mkutano huu wa 19 ambao umemalizika salama na kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, nawashukuru watendaji wote wa Serikali wakiongozwa na Makatibu Wakuu kwa juhudi zao zilizoliwezesha Baraza kuendesha shughuli zake kwa ufanisi katika kipindi hiki. Pia, namshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wote wa Baraza hili kwa maandalizi mazuri ya Mkutano huu. Aidha, nawashukuru Wanahabari wote na Wakalimani wa lugha ya alama kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya za kuwaelewesha wananchi wetu yanayotokea katika Baraza hili.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa heshima na kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako Tukufu hadi siku ya Jumatano tarehe 13 Mei, 2015 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakushukuru sana kwa hotuba yako hii ya kutufungia mkutano wetu huu wa 19 ambao tunaoumaliza leo majira haya kama saa 9:00.

Nawashukuru wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa na kuwashukuru watendaji kwa kutusaidia sana wakiongozwa na Katibu. Narejea kuwashukuru tena Waandishi wetu wa habari ambao wamekuwa nasi kwa muda wote wa mkutano huu, kawaida ya mikutano hii inakuwa ni kama ya wiki mbili lakini mara hii imekuwa wiki tatu kamili, ambazo muda wote tumekuwa hapa tukifanya shughuli kwa ajili ya wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, sasa basi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya kuahirisha Baraza hili hadi tarehe 13 siku ya Jumatano, mwezi wa Mei, saa 3:00 wainue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha mkutano huu, naomba kutoa tangazo moja dogo sana. Waheshimiwa Wajumbe wa upande wa CCM wanaombwa wabakie kwa dakika kama tano tu humu ndani mara baada ya kuahirisha Kikao hichi. Nashukuru kwa taarifa hiyo. Sasa Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuahirisha Mkutano huu hadi tarehe 13 siku ya Jumatano, mwezi wa Mei mwaka 2015 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8:42 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 13/05/2015 saa 3:00 asubuhi)

WIMBO WA TAIFA